# "UCHAMBUZI LINGANISHI WA MAUDHUI NA MTINDO BAINA YA NGANO ZA WASWAHILI NA WAKURIA".

NA

MIRIAM BAGENI MARWA

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA M. A. KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

1987

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

University of NAIROBI Library
0428530 0

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Afr
PN
989
.K4M3
C.4

MIRIAM BAGENI MARWA
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu".

DKT. JAY KITSAO

PROFESA KAREGA MUTAHI
(Mwenye Kiti)

UKURASA

YALIYOMO i

Shukrani iii

Muhtasari v

## SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi 1

1.2 Somo la utafiti 2

1.3 Lengo la utafiti 3

1.4 Sababu za kuchagua somo hili 4

1.5 Upeo wa Tasnifu 4

1.6 Msingi wa Nadharia 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili 9

1.8 Njia za utafiti 11

1.9 Tanbihi 13

## SURA YA PILI

2.0 Uchambuzi wa maudhui na mtindo baina ya ngano za Waswahili na Wakuria 14

2.1 Utangulizi 14

2.2 Uhusiano baina ya mtindo na maudhui 15

2.3.0 Uchambuzi wa ngano 18

2.3.1 Sungura na fisi 20

2.3.2 Kinungu Maria 26

2.3.3 Mtu na Mkewe 29

2.4.0 Uchambuzi wa ngano za Wakuria 34

2.4.1 Mama na Sungura 34

UKURASA

2.4.2 Wesanganache 38

2.4.3 Nyanya na watoto 41

2.5 Tanbihi 44

SURA YA TATU

3.0 Ulinganishi wa maudhui na mtindo 45

3.1 Utangulizi 45

3.2 Kufanana kwa maudhui na mtindo 46

3.3 Tofauti katika Maudhui na Mtindo 53

3.4 Hitimisho 57

3.5 Ambatisho 61

3.6 Marejeleo 97

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa Walimu Wangu, Profesa Karega Mutahi na Dkt. Jay Kitsao walionisimamia katika kazi hii. Wao walinipa moyo pale nilipokuwa naanza kukata tamaa na kunirudi nilipopotoka kitaaluma.

Pia shukrani zangu nazitoa kwa wahadhiri na Wanafunzi katika Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Nairobi, hasa Dkt. Mohamed Bakari, Mwalimu Kazungu Kadenge na Kithaka wa Mberia; kama si wao labda nisingalipata nafasi ya kuiandika tasnifu hii. Sikumsahau Ali Wasi Mwabaya ambaye msaada wake umeniwezesha kuikamilisha kazi hii.

Nawashukuru wahojiwa wote niliowahoji kutoka jamii ya Waswahili na Wakuria. Bila wao ingalikuwa vigumu kukusanya ngano zilizomo katika tasnifu hii. Namshukuru Sheikh Nabahany ambaye alinieleza mengi kuhusu ngano za Waswahili. Pia namshukuru Mzee Marwa ambaye alinitambia ngano za Wakuria zilizomo katika tasnifu hii.

Natoa shukrani kwa wafanya kazi wengine wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, na Wahudumu wa Maktaba na jumuia ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi, kwa ushirikiano wao ulioyapa mazingira ya Chuo mandhari ya kitaaluma. Hali kama hii iliniwezesha kuzingatia kazi yangu kwa makini zaidi.

Nawashukuru jamaa na Marafiki ambao daima hawakukoma kunipa moyo, hasa Ndugu David K. Marwa ambaye tangu tukiwa wadogo amenihimiza nisome sana. Nawashukuru Major na Bibi Manyara walionihifadhi katika maskani yao. Namshukuru kwa dhati Bi Caren Angima tuliyekaa pamoja kwa muda wote niliokuwa nikiifanya kazi hii. Ukarimu na uchesi wake ulinipa moyo pale nilipokuwa naanza kufifia. Sikuwasahau wanafunzi wenzan tulioungana kuvuta kamba pamoja kwa nguvu bila kukata tamaa.

Nashukuru shirika la German Academic Exchange Service (DAAD) kwa kuyagaramia masomo yangu, pamoja na mahitaji mengine ya kifedha kuhusu tasnifu hii.

Natoa shukrani zangu kwa wazazi wangu ambao kwa ushirikiano na subira zao wameniwezesha kufika nilipo sasa. Pia nawashukuru kwa kunifundisha mengi kuhusu jamii yangu, Hayo waliyonifundisha yamekuwa ni muhimu katika kuimaliza tasnifu hii.

Mwisho lakini si akali, natoa shukrani za dhati na kuonyesha fadhila kwa watoto wangu wapenzi Chacha na Marwa, ambao ingawa bado wachanga waliweza kuvumilia ukiwa wa kumkosa mama ili niimalize kazi hii Namshukuru mtuliza nadhari yangu, Mume wangu Dr. J.M. Mwita; kama si yeye nisingerudi chuoni.

Siwezi kumsahau Bi. Lydia Mungai ambaye kwa usanifu na ufasaha, ameipiga taipu tasnifu hii.

## MUHTASARI

Tasnifu hii ni Uchambuzi linganishi wa Mtindo na maudhui baina ya ngano za Waswahili na Wakuria. Hivyo basi huu ni uchambuzi wa fasihi simulizi, ambapo tunashughulikia ngano peke yake.

Fasihi simulizi inazo tanzu nyingi, baadhi yake ni nyimbo, vitendawili na ushairi. Tanzu hizi zaweza kujisimamia zenyewe. Kwa sababu hii hatuwezi kuzichambua zote kwa pamoja. Hata hivyo ni muhimu kujua kwamba, tanzu za fasihi simulizi huingiliana. Kwa mfano katika ngano kuna nyimbo mara kwa mara.

Mahusiko yetu katika ngano hizi, ni kuchambua maudhui na mtindo. Tusemapo mtindo, tunamaanisha usanifu wa lugha inayotumiwa na wasimulizi wa ngano ili waweze kuwasilisha ujumbe wao kwa wasikilizaji. Maudhui kwa upande mwingine ni ule ujumbe unaotolewa kwa ajili ya jamii. Kwa kuwa fasihi simulizi kama fasihi andishi inamhusu binadamu, kigezo tutakachotumia kupimia kazi hii ni msingi wa nadharia ya ki-Marx.

Sura ya kwanza ni utangulizi ambao unaeleza mahusiko yetu katika tasnifu hii. Pia inaonyesha sababu za kulichagua somo hili, yaliyoandikwa kuhusu mada ya kazi hii na njia za utafiti zilizotumiwa kufanya utafiti wenyewe.

Sura ya pili ni uchambuzi wa ngano za Waswahili na Wakuria. Kabla ya uchambuzi, kuna utagulizi ambao

unaeleza mahusiko yetu katika sura hii, pamoja na kueleza kwa muhtasari tu, uhusiano ulioko baina ya mtindo na maudhui.

Baada ya utangulizi huo, tunaingilia uchambuzi wenyewe. Uchambuzi huu, umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imechukua uchambuzi wa ngano za Waswahili. Ngano hizi ni kama zifuatavyo;

(1) Sungura na Fisi

(2) Kinungu Maria

(3) Mtu na Mkewe

Sehemu ya pili imechukua uchambuzi wa ngano za Wakuria. Ngano hizi ni kama zifuatavyo;

(1) Mama na Sungura

(2) Wesanganache

(3) Nyanya na watoto

Sura ya tatu ni ulinganishi wa maudhui na mtindo wa ngano ambazo tumezichambua. Kabla ya ulinganishi wenyewe. Kuna utangulizi ambao unaeleza sababu za kuwa na ulinganishi huu. Ulinganishi huu umegawanyika katika sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza imechukua kufanana kwa maudhui na mtindo baina ya ngano za Waswahili na Wakuria. Sehemu ya pili imechukuwa tofauti zilizoko baina ya ngano za jamii hizi, tukizingatia maudhui na mtindo.

Baada ya ulinganishi huu, tuna hitimisho. Katika hitimisho uamzi na mapendekezo yetu yanajitokeza

Mwisho kabisa kuna ambatisho ambalo ni uambatanishiwa ngano zote tulizozichambua. Ngano hizi zimepangwa kama ifuatavyo; kwanza kuna ngano za Waswahili, zikifuatiwa na ngano za Wakuria katika lugha ya Kikuria. Mwisho ni tafsiri ya ngano za Wakuria katika lugha ya Kiswahili.

## 1.1 UTANGULIZI

Fasihi simulizi ni sanaa ya maneno ya mdomoni ambayo haiwezi kutengwa na uigizaji. Kwa mfano mtu anaposimulia ngano juu ya sungura na fisi mara nyingi huigiz sauti na vitendo vya wanyama hawa wawili. Pamoja na uigizaji huu, fasihi simulizi huwa na hadhira kila wakati.[1]

Ijapokuwa fasihi simulizi imeanza kupewa umuhimu kama somo katika mashule na vyuo hivi majuzi tunajua kwamba ilikuweko tangu zamani. Fasihi simulizi ilitokea katika jamii na bado inaendelea kutokea mumo humo. Fasihi simulizi huibuka na kuoana na utamaduni wa jamii ambao hukua kwa msingi wa uzalishaji mali ukiambatana na jumlisho la amali zao.[2]

Katika msingi huu, tunaona kuwa fasihi simulizi ni zao na amana ya jamii ambayo ina wajibu muhimu sana. Fasihi simulizi huratibu tajriba za watu katika jamii, matarajio yao, mahusiano yao na binadamu wenzao pamoja na kuonyesha harakati zao katika kuthibiti mazingira yao. Pia fasihi simulizi inatumika kama chombo mashuhuri cha kuhifadhi, kulinda na kuendeleza amali za jamii. Amali hizi ni kama vile ari na juhudi za kazi pamoja na uendelezaji wa sehemu kadhaa za utamaduni kama vile mambo ya ndoa, uzazi na mafunzo mbalimbali yanayoingiliana na mazingira ya jamii.

Fasihi simulizi ni jumlisho la tanzu kama vile ngano, vitendawili, methali, nyimbo na ushairi.

Katika tanzu hizi, fasihi simulizi inakuwa, chombo cha mawasiliano ikitumia lugha kama malighafi. Fasihi simulizi hutumia, lugha kama chombo muhimu cha kuwasilishia ujumbe unaodhamiriwa.

Fasihi simulizi kama sanaa ya maneno ya mdomoni daima iko hai. Hivi ni kusema kwamba inageuka kadiri historia ya jamii inayoizaa inavyogeuka. Katika kugeuka huku, fasihi simulizi inakidhi haja na mabadiliko ya mifumo ya jamii kiuchumi na kisasa.

## 1.2 SOMO LA UTAFITI

Mada ya tasnifu hii ni Uchambuzi Linganishi wa Maudhui na Mtindo baina ya Ngano za Waswahili na Wakuria.

Kwa kuwa ngano ni utanzu mmoja wa fasihi simulizi, somo letu tunaliona kama fasihi simulizi. Fasihi simulizi kama fasihi andishi ni zao la jamii na inashughulikia taratibu za jamii katika jumuiya maalum. Taratibu hizi ni kama vile, mahusiano baina ya watu, shughuli za kiuchumi na kisiasa. Fasihi hii inaposhughulika na taratibu za jamii inakuwa chombo cha mawasiliano ya hisia za jamii kwa jumla. Mathalani fasihi simulizi inaweza kutuonyesha vile jamii inavyohisi mazingira yake pamoja na matarajio yake. Pamoja na hayo, fasihi simulizi inafunza juu ya umuhimu wa mila na utamaduni wa jamii, busara, uadilifu, historia na mengine mengi.

Kwa sababu hii, fasihi simulizi inajitokeza kama sanaa inyotoa mwongozo wa tabia njema na mahusiano bora baina ya watu katika jamii. Ndiposa katika tasnifu hii, tunataka kuthibitisha kama kweli fasihi simulizi kama sanaa ilitoa mwongozo wa mahusiano baina ya watu katika jamii ambazo tunazishughulikia.

## 1.3 LENGO LA TASNIFU

Lengo letu katika tasnifu hii ni kuchambua na kisha kulinganisha maudhui na mtindo wa ngano baina ya jamii ambazo tumezitaja. Lengo la kuchambua maudhui na mtindo ni kutaka kujua ujumbe uliomo kwenye ngano za Waswahili na Wakuria, pamoja na mbinu walizozitumia wasanii wa jamii hizi mbili ili kuwasilisha ujumbe wao. Tumelinganisha maudhui na mtindo kwa madhumuni ya kutaka kuona tafauti na kufanana kwa jamii hizi ambazo tunajua kuwa kijiografia hazikaribiani.

Pia tunataka kujua kama fasihi simulizi ni kioo cha mahusiano halisi ya watu katika mfumo wa kijamii na kiuchumi wa ujima. Pamoja na hayo tunataka kujua kama fasihi simulizi iliwakilisha itikadi ya mfumo wa kiuchumi, kijamii na kisiasa, pamoja na kumulika mabadiliko ya maendeleo yaliyotokea miaka nenda miaka rudi katika mahusiano ya watu ambayo yalitokana na kuwepo kwa nyenzo za kuzalisha mali.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Fasihi simulizi ni somo ambalo limeanza kukua na kupewa nguvu katika mashule na kwenye vyuo hivi majuzi. Kwa sababu hii tunaona kuwa kuna uhaba wa kazi za somo hili, hivyo bado fasihi simulizi inahitaji utafiti mwingi hasa utakaochangia na kukuza fasihi ya Kiswahili. Ili tuweze kutoa mchango wetu, tumetafsiri na kuchambua ngano za Wakuria katika lugha ya Kiswahili.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Sababu ya pili ni kuwa, tunataka kuona picha kamili ya hali halisi ya maisha ya kila siku ya wakati fulani katika jamii ya Waswahili na Wakuria, na kama leo hali hiyo imebadilika. Jambo hili tumelichunguza katika uchambuzi wetu ambao umezingatia maudhui na mtindo wa ngano zao. Pia katika kufanya hivyo tunataka kuona kama jamii hizi zinafanana au kutofautiana.

Mwisho ni kuwa, ikiwa ngano hizi zilikuwa na ujumbe muhimu hapo zamani ambao ulikuwa na manufaa kwa jamii, tunaamini kuwa ujumbe huo bado unaweza kuwa wa manufaa hivi sasa. Tunazichambua ngano hizi tukiwa na lengo la kuonyesha umuhimu wake katika jamii.

## 1.5 UPEO WA TASNIFU

Katika tasnifu hii tumezingatia utanzu mmoja tu

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

wa fasihi simulizi ambapo tumechambua na kulinganisha maudhui na mtindo wa ngano za Waswahili na Wakuria. Tumefanya hivi kwa sababu kila utanzu wa fasihi simulizi una uwezo wa kujisimamia pia wakati wetu si mwingi wa kuturuhusu kuzingatia tanzu zaidi ya moja. Ngano zetu ni zile za paukwa ... pakawa. Zenye wahusika wanyama na wanadamu. Kwa upande wa Waswahili tumeacha ngano zenye athari za kigeni.

Tulikusanya ngano kutoka jamii mbili ambazo tumezitaja. Hatukuwa na idadi maalum ya ngano ambazo tulizikusanya bali tulikusanya ngano kwa kuchagua zile ambazo zingetufaa katika tasnifu hii. Baadaye tukachukua ngano sita peke yake, tatu kwa upande wa Waswahili na tatu kwa upande wa Wakuria.

Katika tasnifu hii, habari zote ambazo zimedondolewa au kujadiliwa katika lugha ya Kikuria zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa mtindo tumezingatia dhana ambazo hutumiwa na wasanii ili kuwasilisha ujumbe unaodhaminiwa na kudhihirisha ufundi na ufasaha wa lugha wanayoitumia. Dhana hizi ni kama vile istiara, tashbihi, taswira, tashhisi na nyingine nyingi.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Katika tasnifu hii, tunachambua maudhui na mtindo baina ya jamii ambazo tumezitaja. Kwa sababu hii tunakuwa na vigezo viwili vya kupimia kazi hii. Kwa upande wa mtindo, tunatumia dhana ya Mcintosh kuhusu mtindo. Mcintosh anasema kuwa;

> Mtindo ni vile mtu anavyozungumza
> Kila siku, ikiwa anatazama au hatazami,
> akijaza makosa au bila kujaza makosa....[3]

Kwake McIntosh, hakuna sarufi mbaya. Mtu azungumzavyo huo ndio mtindo wake. Jambo linalojitokeza hapa, ni kuwa mtindo huandamana na lugha. Kwa hivyo mahusiko yetu juu ya mtindo yanakuwa ni kuangalia lugha wanayoitumia wasimulizi wa ngano na vile wanavyoitumia. Kwa upande wa maudhui, tunatumia nadharia ya Marx kuhusu fasihi kama kigezo chetu. Nadharia hii inajitokeza katika kitabu cha Marx na Engels, ON LITERATURE AND ART.[4] Kulingana na nadharia ya Marx, fasihi iwe simulizi au andishi inamhusu binadamu. Fasihi ni sanaa inayotumia maneno ili kumlika maisha ya binadamu. Fasihi inapomulika maisha ya binadamu, inaonyesha uhusiano ulioko katika jamii baina ya mtu na wenzake. Hii ndiyo sababu ya kuona fasihi kama kioo cha jamii ambacho hutuchorea hali halisi ya maisha

katika jamii. Hivyo mwandishi au msimulizi atakayefaulu ni lazima amulike na kumweleza binadamu anavyoishi katika maisha yake ya kila siku. Kueleza binadamu anavyoishi katika maisha ndio uhalisi kulingana na nadharia ya Marx kuhusu fasihi.

Pamoja na hayo, nadharia ya Marx inatuonyesha vile jamii imeundwa. Kwa mfano jamii inaweza kuwa katika hali ya matabaka. Katika jamii yenye matabaka, fasihi iwe andishi au simulizi ni lazima iwe na msimamo.[5] Hivyo kila tabaka linakuwa na fasihi inayotetea maslahi yake. Kwa mfano makabaila walikuwa na fasihi yao, yenye kutetea ukabaila kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine matwana nao waliupinga ukabaila wakitumia fasihi simulizi.

Mulokozi (1982:40) anasema;

> Katika hali ya kitabaka, tabaka lililokuwa likitawala liliandika mashairi ya wosia ambayo yalikuwa na lengo la kushawishi na kushauri tabaka lililotawaliwa kukubali hali ya Serikali ya ukabaila wa Kiislamu kwa upande mwingine - tabaka la watwana lilitoa maoni yao kwa kupitia fasihi simulizi.[6]

Ukweli wa jambo hili, unatokana na ukweli mwingine kuwa, fasihi kama njia ya kuwasilisha itikadi ya tabaka fulani ni silaha ya kuwaunga mkono wanaonyonywa, ama kuwaunga mkono wanyonyaji. Hivi ni kusema kwamba

katika jamii yenye mfumo wa kikabaila, makabaila huwa na fasihi yao wenyewe yenye lengo la kuimarisha na kudumisha ukabaila. Kwa upande wao matwana, nao huwa na fasihi yao ya kupinga ukabaila na kuwasilisha itikadi ya kupambana na makabaila wanaonyonya jasho lao.

Mulokozi (1982:30) anasema kuwa katika pwani ya Afrika Mashariki kulikuwa na matabaka.

> Tabaka na harakati za kitabaka zilikuwepo kitambo hata kabla ya kuwasili Wareno, na ushahidi wa jambo hili unapatikana katika maandishi ya karne ya kumi hadi ya kumi na nne ya Waarabu....[7]

Tunapozingatia maelezo ya Mulokozi, tunaona kuwa, yanaingiliana na nadharia ya Marx ambayo inaonyesha waziwazi uhusiano ulioko katika jamii, baina ya mtu na jamii yake, pia kati ya tabaka moja na jingine. Uhusiano huu huwa na mwongozo katika fasihi ambayo hutumiwa kuwasilisha itikadi ya kila tabaka.

Vilevile tunaona kuwa fasihi simulizi kama fasihi andishi, mbali na kuwasilisha itikadi ya mfumo wa kijamii na kisiasa, inamulika mabadiliko ya maendeleo yaliyokuwa yakitokea miaka nenda rudi katika mahusiano ya watu kutokana na kukua kwa nyenzo za kuzalisha mali. Fasihi simulizi inavyojitokeza ni kitovu cha maendeleo ya mwanadamu katika pande zote za historia. Ndiyo maana

tumeichagua nadharia hii ya Marx kuhusu fasihi, kuwa msingi wa tasnifu hii.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi nyingizilizotangulia kuchapishwa juu ya fasihi simulizi ya jamii mbalimbali za Kiafrika zilitayarishwa na wageni ambao mara nyingi hawakuwa na ujuzi kamili wa utamaduni wa watu waliowasimulia. Mara nyingi waandishi kama hawa walitosheka tu kwa kukusanya mambo machache ya hapa na pale kuhusu jamii fulani na kwa ushahidi kama huo wakaamua mambo chungu nzima juu ya dini, imani, historia na hata Elimu ya jamii hizo. Jambo hili limeathiri sana fasihi simulizi ya jamii ambazo tumeshughulikia katika tasnifu hii.

Tukianza na jamii ya Waswahili, tunaona kuwa, fasihi simulizi ya jamii hii ilishughulikiwa kwanza na wageni ambao wengi wao walikuwa wamisheni na watawala wa kikoloni. Hawa walikusanya kazi nyingi sana za fasihi simulizi. Kazi waliyoifanya ina umuhimu kwa sababu tunaweza kuitumia kufanya uchunguzi zaidi katika somo hili la fasihi simulizi.

Tofauti iliyoko baina ya kazi za fasihi simulizi walizozifanya wamisheni na watawala wa kikoloni, na hii tunayonuia kuifanya ni kuwa, sisi katika utafiti wetu, tumechambua maudhui na mtindo wa ngano za Waswahili. Baadaye tumelinganisha maudhui na mtindo

unaojitokeza katika ngano za Wakuria.

Lengo letu limetofautiana na lile la Wamisheni na Watawala wa Kikoloni ambao, lengo lao lilikuwa kukusanya na kutafsiri tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya kiswahili hadi kiingereza.

Fasihi simulizi ya Waswahili imeshughulikiwa hivi karibuni. Kwa mfano Mwabaya, A.W. (1985) ameshughulikia, Fasihi Simulizi Miongoni Mwa Wajomvu. Kama tujuavyo Wajomvu ni jamii ya Kiswahili. Kazi hii ni uhakiki wa maudhui katika ngano za Wajomvu. Kwa kiasi fulani kazi hii inaingiliana na yetu ila sisi tumepiga hatua moja zaidi na kuchambua ngano za jamii ya Waswahili na Wakuria Kimaudhui na Kimtindo.

Kazi nyingine ya fasihi simulizi ya Waswahili ni ile ya Fasihi Simulizi Zanzibar (1983). Kazi hii imeshughulikiwa na watu wanne, Ameir, I.H. Ruhman, M.N. Ali, M.M na Asia, A.M. na imezingatia karibu tanzu zote za fasihi simulizi kama vile, methali, vitendawili, hadithi na nyimbo. Hivyo kazi hii imezingatia fasihi simulizi kwa jumla.

Inatofautiana na yetu kwa sababu sisi tuna lengo la kuchambua ngano za jamii mbili tofauti tukiwa na lengo la kulinganisha maudhui na mtindo wa ngano za jamii hizi.

Tunapozingatia fasihi simulizi ya Waswahili, inatokea kuwa mengi yameshughulikiwa, lakini yaliyowahi kushughulikiwa hayatoshi kusimamisha utafiti zaidi wa

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

fasihi simulizi ya Waswahili hasa tukikumbuka kwamba, fasihi hubadilika kulingana na wakati.

Kuhusu fasihi simulizi ya Wakuria tunaweza kusema kuwa ni machache sana yajulikanayo juu yake. Kazi inayohusiana na fasihi simulizi ya Wakuria ni ile ya Kingdon, D. (1959). <u>Hadithi ya Abakuria wa Tanganyi</u> Katika kazi hii Kingdon alikusanya ngano za Kikuria na baadaye akazitafsiri katika lugha ya Kiswahili. Kaz yake inashabihiana na yetu kwa kuwa hata sisi tumetafsi ngano hizi kutoka lugha ya Kikuria hadi Kiswahili. Tofauti iliyoko ni kuwa tumechambua ngano tulizozikusan kimaudhui na kimtindo.

Odaga (1984) amegusia kwa mseto fasihi simulizi ya Wakuria. Yeye kama Kingdon, D. lengo lake lilikuwa kukusanya ngano na baadaye akazitafsiri katika lugha ya Kiingereza. Tofauti iliyoko baina ya kazi yetu na yake ni kama iliyo katika kazi ya Kingdon, kwani sisi tumechambua ngano za Wakuria kimaudhui na kimtindo.

Tunapolinganisha jamii hizi mbili, tunaona kuwa jamii ya Wakuria haina kazi nyingi juu ya fasihi simuli Na zile chache ambazo zimefanywa Zinahitaji kufafanuli zaidi.

## 1.8 <u>NJIA ZA UTAFITI</u>

Utafiti wetu tuliufanya Mombasa na sehemu ya Kur Wilayani Nyanza Kusini. Watu tuliowahoji kutoka pande zote mbili walikuwa wenyeji wa lugha na utamaduni wa jamii zinazohusika.

Pia tuliwahoji watu wenye ujuzi wa kusimulia na kufafanua maana ya ngano. Katika utafiti huu tulitumia Maktaba ya chuo kikuu cha Nairobi.

Hatua hizi zifuatazo ndizo zilizotuongoza katika kufanya utafiti wetu.

(1) Tulirekodi ngano tulizozihitaji katika tasnifu hii.

(2) Tulitumia daftari la utafiti kwa kuandikia yale yote tuliyoyaona na kusikia kuhusu ngano.

(3) Kwa kuwa hakuna fasihi isiyobadilika, tulitaka kujua kama fasihi simulizi imebadilika miongoni mwa jamii hizi. Hivyo tuligawanya wahojiwa wetu katika makundi matano kulingana na umri wao. Pamoja na umri, ni Uana, yaani wahojiwa wetu walikuwa wanaume kwa wanawake.

Makundi tofauti tuliyoyahoji kulingana na umri ni kama yafuatavyo.

| | | |
|---|---|---|
| Miaka | 15 - | 25 |
| " | 25 - | 35 |
| " | 35 - | 45 |
| " | 45 - | 55 |
| " | 55 ——— | |

Sababu ya kufanya hivi ni kuwa, kimaisha, makundi tofauti kiumri huwa na tajriba tofauti kuhusu vile fasihi simulizi ilivyokuwa na vile imebadilika sasa.

1.9 TANBIHI

1. Odaga, A.B. (1984) Yesterday's Today: The study of Oral Literature. Lake Publishers and Enterprises Kisumu.

2. Khamis, S.A. (1983) "Nafasi ya Fasihi Simulizi Katika Jamii ya Kitanzania". Makala katika mulika No. 15. Jarida la Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3. Soma M.A. Thesis ya Kitsao, J. (1975) Astylistic Approach Adopted for the Study of written Swahili prose Texts.

4. Soma Kitabu cha Marx, C. na Engels, F. On Literature and Art, Progress Publishers Moscow (1978).

5. ____________ Kama 4 hapo juu.

6. Mulokozi, M.M. (1982) "Protest and Resistnance in Swahili poetry 1660 - 1885". Makala katika Kiswahili Vol. 49/1 March. Janda la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

7. ____________ Kama 6 hapo juu.

# SURA YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAUDHUI NA MTINDO BAINA YA NGANO ZA WASWAHILI NA WAKURIA

## 2.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tunachambua maudhui na mtindo katika ngano za jamii ambazo tumezitaja. Neno maudhui tunalitumia kumaanisha ujumbe unaosheheniwa na ngano. Tusemapo mtindo tunamaanisha mbinu mbalimbali wanazozitumia wasimulizi kuwasilisha ujumbe huo. Kwa kufanya hivyo tutakuwa na nafasi ya kuonyesha vile fasihi simulizi ilivyo chombo cha mawasiliano katika jamii kwani ngano ni utanzu mmoja wa fasihi simulizi.

Ili tuweze kutekeleza wajibu huu, tumeigawanya sura hii katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni kuhusu maudhui na mtindo. Hapa tunataka kuonyesha uhusiano ulioko baina ya mtindo na maudhui. Hili tutalifanya kwa sababu mahusiko yetu makubwa katika sura hii kama tulivyosema ni uchambuzi wa maudhui na mtindo. Sehemu ya pili ni uchambuzi wa ngano sita, tatu zikiwa za jamii ya Waswahili, na tatu za jamii ya Wakuria. Ngano zenyewe ni kama zifuatavyo;

(1) Sungura na Fisi

(2) Kinungu Maria

(3) Mtu na Mkewe

(4) Mama na sungura

(5) Wesanganache

(6) Nyanya na watoto

Ngano za kwanza tatu ndizo za Kiswahili na zinazobaki ndizo ngano za Kikuria.

## 2.2 UHUSIANO BAINA YA MTINDO NA MAUDHUI

Maudhui na mtindo ni fani mbili za fasihi amba hujenga kazi za kifashi. Wanafasihi wengi ambao wamezama katika uchunguzi wa fasihi wamesema kuwa, mtindo na maudhui huambatana na kutegemeana. Hivi ni kusema kwamba, katika kazi za kifasihi huwa kuna ujumbe ambao huwasilishwa unapodhamiriwa kwa kutumia mbinu fulani. Kwa njia nyingine tunaweza kusema kuwa, fasihi simulizi kama fasihi andishi huwa na mawazo pamoja na ufundi na usanii kama anavyosema Khamis S.A. (1983).

> Fasihi simulizi si fikra na mawazo tu, pamoja na hayo ni ufundi na usanii uliomo. Usanii huo, huambatana sana na mcharazo wa lugha ambao unajidhirisha katika vivuli mbalimbali vya maana, sitiari, tamathali na picha mbalimbali zinazochorwa kutegemea tamaduni za Wasanii wetu.[1]

Kwa kuwa fasihi simulizi si fikra na wawazo tu lazima kuwepo na kiungo kingine kama ambavyo tumeona ha juu. Mohamed, S.A. (1981) anasema, sharti kuwepo na muundo, usanii wa lugha, ubunaji wa visa na vitu, ufiny wa wahusika na wasilisho la wakati, majira na mabadilik ya mazingira, ikibidi katika hali ya kumteka msomaji au msikilizaji bila kumpa nafasi ya kuvuta pumzi. Jumla y mambo haya yote tunaweza kuyaona kama mtindo na ndiyo

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

maana tumesema kuwa mtindo unaingiliana na maudhui.

Mjadala ambao tumeuendeleza hapo juu kuhusu kuingiliana kwa maudhui na mtindo, unaweza kuendelezwa zaidi na maneno ya Mohamed, S.A. (1981) asemaye kuwa;

> Mtindo na Maudhui lazima ipime sawa katika mizani ya fasihi, yaani mtindo usijitokeza mno kuziba kinachozungumziwa au mkazo usiwe mkubwa kwa kinachozungumziwa hata ikasahauliwa fani ya kufanya kazi ya fasihi ina ukavu wa mawazo yasiyolainishwa yakaweza kumezwa.[2]

Kutokana na nukuu hii, tunaona ushahidi mwingine kuwa licha ya maudhui kuwa muhimu zaidi katika fasihi yoyote ile, yanatengemea mtindo na mtindo nao kwa upande mwingine unategemea maudhui. Uhusiano huu unamaanisha kuwa maudhui na mtindo daima huambatana na kuwa fani hizi haziwezi kutenganishwa. Labda ukweli huu kuhusu mtindo na maudhui ndio ulimfanya Abdilatif Abdalla (1980) aseme hivi;

> Ala ya kwanza iliyo muhimu katika sanaa itumiayo maneno ni umbuji wa lugha. Ili msanii aweze kumtia mkononi msomaji au msikilizaji wake na kuweza kumweka kitako kwa muda mrefu na akawa yuasoma au kusikiliza kwa makini na uzingatifu, bila ya msomaji au msikilizaji huyo kuchoshwa naye, badala yake akawa anayaonea raha hayo yatokayo kwa msanii na akawa

> hataki yamalizike, msanii huyo anahitaji kuwa na ukwasi wa lugha teule, pamoja na kuzijua mbinu za kutumia ukwasi huo kwa namna itakayoathiri vilvyo.[3]

Maneno ya Abdilatif Abdalla (1980) yametuelekeza kwenye kipengele kingine cha fasihi kwa jumla. Msimulizi au mwandishi sharti atumie na kupanga lugha yake vilivyo. Aipange kwa njia ambayo itamwezesha kuwasiliana na wasikilizaji au wasomaji wake kwa njia ya kuvutia na ambayo itawafanya wasikilize au wausome ujumbe wake. Lugha **kwa njia** hii inakuwa malighafi ya kuumba sanaa ya fasihi. Kwa kusema hivi tuna maana kwamba lugha ina uhusiano wa karibu sana na maudhui. Jambo hili kwa kiasi kikubwa la tuonyesha kuwa maudhui na mtindo hutegemeana.

Katika kuzungumzia uhusiano ulioko baina ya mtindo na maudhui, Fischer, E. (1959: 131) anasema;

> Maudhui si kile kilichoelezwa peke yake, bali njisi kilivyoelezwa, katika mkutadha gani na kutegemea kiwango cha hisia na mtu binafsi na jumuiya kwa jumla.[4]

Jambo linalojitokeza katika nukuu hii ni kwamba Fischer, anasema kuwa maudhui ni mtindo. Lakini swali ambalo twapasa kujiuliza ni kama maudhui ni mtindo. Jibu ni kwamba maudhui si mtindo, bali maudhui na mtindo hutegemeana katika kujenga kazi za kifasihi. Jambo ambalo

tunakubaliana nalo ni kwamba maudhui huwa katika mktadha fulani kutegemea kiwango cha hisia za mwandishi au msimulizi na mazingira ya jamii yake.

Fasihi iwe simulizi au andishi sharti iwe na utaratibu maalum. Utaratibu huu ni wa aina nyingi. Kwa mfano kutumia lugha kisanaa kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe anaoudhamiria msanii. Pili msanii atatafuta njia za kuvutia hadhira yake, jambo ambalo litaifanya hadhira yake, kusikiliza au kuusoma ujumbe alio nao msanii. Katika mambo haya ambayo yanaingiliana na lugha tunaona kuwa mtindo unaingiliana na maudhui na kuwa mtindo na maudhui vyote hutegemea lugha.

Kutokana na maelezo haya kuhusu maudhui na mtindo imebainika kuwa mtindo na maudhui huathiriana na kwamba lugha ndiyo chombo muhimu cha kuunganisha mtindo na maudhui. Katika tasnifu hii, tutakuwa tunazingatia ujumbe upatikanao katika ngano za Waswahili na Wakuria pamoja na mbinu wanazozitumia wasimulizi wao kuwasilisha ujumbe huo.

## 2.3.0 UCHAMBUZI WA NGANO

Katika uchambuzi huu tutachukuwa neno mtindo kumaanisha ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Hivi ni kusema kwamba, kufaulu au kutofaulu kwa msanii katika mtindo anaoutumia kutategemea uteuzi

wake wa maneno mbalimbali na vile anavyoyatumia. Ja hili ni muhimu kwa sababu fasihi simulizi kama fasil andishi ni sanaa ambayo hutumia maneno ambayo hutaml Hivyo basi tunaona kuwa, mtindo hutegemea sana matu ya lugha na uteuzi wa maneno katika muktadha wa tas hii.

Kipengele cha lugha ni muhimu sana kwa sab ndicho hutofautisha fasihi na sanaa nyinginezo, kam vile uchoraji ambao kipengele chake muhimu ni kalam rangi, kipande cha karatasi au nguo. Lugha ndiyo mizizi ya kazi za kifasihi, bila lugha hatuwezi kuw fasihi. Lugha ndiyo hutumiwa na msanii kuyaelezea mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya ubunaji na ufa Mambo yale anayoyaeleza ndiyo tunayoyachukulia kuwa maudhui.

Matumizi ya lugha ni ya aina nyingi. Kati lugha kuna tamathali za wahusika hasa tukichukulia zao, uchaguzi wa msamiati, miundo ya sentensi, Ufun wa kutoa maelezo hasa ya wahusika, mandhari, matuki utamu wa lugha yenyewe itumiwayo.

Hayo ambayo tumeyasema kwa kifupi ndiyo ya kuwa kigezo chetu cha kuchambua ngano tulizozikusan kimaudhui na kimtindo. Katika uchambuzi huu, tutaa na ngano za Kiswahili zikiwa ni Sungura na Fisi, Kinungu Maria, na Mtu na Mkewe.

## 3.1 SUNGURA NA FISI

Ngano ya Sungura na Fisi ina mambo mengi ambayo tunaweza kuyaona kama maudhui. Kwanza kabisa ngano hii inatuonyesha wakati. Ingawa hakuna miaka wala tarehe, tunaelewa kuwa ni hapo kale. Labda tunaweza kujiuliza kuwa hapo kale kulikuwa na nini?. Jibu tunalipata kutoka kwa wahusika tofauti wa ngano hii. Msimulizi anatuonyesha shughuli muhimu za wakati fulani katika jamii ya Waswahili

Waswahili walikuwa na mashamba. Kazi ya kulima mashamba haya ilitekelezwa kulingana na majira ama misimu fulani, ndiyo maana sungura anasema "rafiki yangu tulime mashamba kwani sasa tunaona mwaka unaenda kwisha, mimi nitapanda migomba na wewe utapanda chumvi".

Kazi nyingine ambaso zinajitokeza katika ngano hii ni kama vile kuteka maji. Tunaelezwa kuwa maji yalitekwa kisimani na kitu kilichotumiwa kuyateka ni kata. Kuwinda, kuvua samaki, kuchunga ng'ombe na kuchanja kuni ni shughuli nyingine walizo zitekeleza Waswahili wa hapo zamani. Kusema kweli hizi ni shughuli ambazo zilitendeka na bado zingali zikitendeka miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika. Ujumbe huu ambao tumeupata kuhusu jamii ya Waswahili ulikuwa ni muhimu katika jamii hii kwa sababu watoto walitayarishwa kimawazo juu ya kazi ama shughuli ambazo walitarajiwa wazitekeleze hasa wakiwa watu wazima.

Tukirudi kwa upande wa mafunzo tunaona kuwa

UNIVERSITY OF NAIROBI

ngano hii inatufundisha juu ya uhusiano baina ya watu. Hapo mbeleni tumewahi kusema kuwa fasihi huzingatia mahusiano baina ya binadamu katika jamii na kwamba kila fasihi huzingatia binadamu hata kama wahusika siyo bina damu.

Katika kufundisha juu ya uhusiano baina ya Wanajamii, Msanii ameigawanya ngano hii katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza tunaona, wahusika wawili yaani Sungura na fisi. Wahusika hawa ni marafiki wa chanda na pete. Katika sehemu ya pili tunaona sungura na wahu wengine kama vile watu, ndege na kisiki. Sehemu hii na imebeba mafunzo kuhusu uhusiano baina ya watu katika j

Muhimu katika ngano hii ni uhusiano wa marafi Mwanzoni mwa ngano tunaambiwa kuwa, sungura na fisi walikuwa marafiki wa chanda na pete. Kwa maneno mengin hawa walikuwa marafiki wakubwa sana ambao ni imani yetu kuwa waliheshimiana. Lakini licha ya urafiki wa kiwang hicho, sungura anamhadaa rafikiye kwa kumwambia apande chumvi. Hapa tunaona sifa moja mbaya ambayo inaweza kuharibu uhusiano baina ya watu walio marafiki.

Katika ngano hii tunaona kuwa, fisi aligundua baadaye kuwa sungura alimdanganya kwa kumwambia apande chumvi ambayo haipandwi. Baada ya kugundua hivyo fisi alitaka kulipiza kisasi kwa kula ndizi za sungura. Mat ni kwamba sungura anamua fisi. Hivyo tunafundishwa kuwa kundanganyana hakufai katika uhusiano wa kirafiki.

Ingawa msimulizi ametumia wanyama hawa tunawe kusema kuwa, katika maisha ya kila siku kuna binadamu

wengi ambao ni sungura hata kuliko sungura wenyewe walivyo. Pia kuna fisi wengi kuliko fisi wenyewe hasa. Hivi ni kusema kuwa wanyama hawa hawajisimamii wenyewe bali wanasimamia wanadamu na tabia zao. Kwa hivyo kutokana na matendo ya sungura na fisi tunapata fundisho kuwa rafiki aweza kumdanganya na kumfanya mwenzake mjinga. Pia kusikiliza na kutenda kulingana na maoni ya marafiki si jambo la busara. Ni muhimu kufikiria kabla ya kutenda jambo ambalo limependekwa na rafiki yako. Kama fisi angelipuuza pendekezo la kupanda chumvi kama alivyopendekeza sungura hangepanda chumvi. Jambo jingine tunalofundishwa hapa ni kwamba mtu anaweza kumgeuka rafiki yake na kumkatia maisha yake, kama sungura alivyomfanyia fisi ambaye alijaribu kumwambia kuwa amemdanganya.

Kwa kutumia sungura, msimulizi ametufundisha kuwa wako baadhi ya wanadamu ambao ni werevu, hasa werevu wa kupoteza wenzao. Hawa hutumia urafiki kuharibia wenzao maisha. Tunaonywa tujiepushe na watu kama hao. Kwa upande mwingine wako wengine wapumbavu ambao hufuata mawaidha ya marafiki wao bila kuyapima na kuona faida na hasara yake. Mwishowe watu kama hawa hutambua makosa yao wakati ambapo hakuna la kufanya ila kuangamia. Hili ni onyo ambalo daima halitabadilika maana kila siku watu hukutana na kuwa marafiki.

Katika sehemu ya pili ya ngano hii, muhusika sungura anaonyeshwa pamoja na wahusika wa aina tofauti. Sungura anakutana na watu, ndege, na kisiki. Katika

uhusiano wake na wahusika hawa, sungura anajitokesa kuwa mwenye ujanja mwingi na mwenye kutania. Kwa mfano sungura anapokutana na watekaji maji anawapatia kata yake kwa nia nzuri, ambapo hatutarajii kuwa baadaye ataitaka tena. Lakini mara tu inapokatika, sungura anaanza kuiomba, akisema "mtanilipa". Hili ni jambo ambalo halipendezi watu na tunaona kuwa sungura kila alipofanya hivyo alipewa ama alilipwa kwa kitu tofauti na kile alichotoa. Matani mara nyingi huudhi ama humfanya mtu aseme au atende jambo bila kujua hasara itakayotokea. Ni kutokana na uhusiano aina hii ambapo tunamwona sungura akimchomea kinyanya nyumba, ilhali yumo humo. Hivyo tunafundishwa kuwa mzaha mzaha mwisho hutumbuka nyongo.

## MTINDO

Kwa upande wa mtindo, msimulizi ametumia mbinu kadhaa kuwaisilisha ujumbe wake. Kwanza ameanza ngano kwa maneno paukwa....pakawa. Haya ndiyo maneno muhimu ya kuhimiza wasikilizaji wanyamaze ili kumpa nafasi ya kutoa ujumbe wake. Baada ya paukwa, tunaona kuwa ngano hii inaanza kwa maneno kama vile "Hapo zamani za kale". Maneno haya ni muhimu kwa sababu yanatuonyesha wakati.

Pamoja na hayo msmulizi ametumia mbinu nyingine nyingi ambazo zinamfanya afaulu kutoa ujumbe wake ambao tumeuona. Ngano hii in wahusika ambao ni wanyama, wanadamu na kisiki. Wale wahusika ambao si binadamu,

"ah sungura mbona wewe migomba yako inakua lakini mimi chumvi yangu hata haijatokeza?".

Mbinu nyingine ambayo imetumiwa katika ngano hii ni matumizi ya misemo. Kwa mfano msimulizi ametumia msemo wa "chanda na pete", kutuonyesha uhusiano baina ya sungura na fisi. Mara mtu achunguzapo maneno ya msemo huu anaona kuwa sungura na fisi walikuwa marafiki sana. Msemo huu unatuchorea picha ya kidole na pete. Pete na kidole daima huwa pamoja, hivyo anatumia taswira kuwasilisha ujumbe wake.

Tashbihi imetumiwa katika ngano hii, pale ambapo msimulizi anasema kuwa tumbo la fisi lilikuwa limejaa kama gunia. Mbinu ya mwisho ambayo imetumiwa katika ngano hii ni ile ya kupiga chuku. Katika ngano tunaelezwa kuwa kinyanya alikuwa akichanja mguu wake ili apate kuni za kupikia kunde zake. Katika hali halisi mtu hawezi kuchanja mguu wake ili aufanye kuni. Hili ni jambo la ngano tu, linalotuonyesha kuwa mama mzee huyu alikuwa hana kuni kabisa.

Haya yote ambayo tumeyazingatia juu ya mtindo yamedhihirisha kuwa utambaji wa ngano unatendwa na watu wenye kuijua jamii yao. Hivyo msimulizi wa ngano hii ametueleza mengi juu ya jamii yake, akitumia mbinu mbalimbali kama ambavyo tumeona. Msimulizi wa ngano hii amejitokeza kama bingwa wa kazi hii ya fasihi na ameisanii vilivyo.

### 2.3.2 KINUNGU MARIA

Fasihi simulizi haiko kwenye ombwe tupu bali hufuata mwelekeo wa jamii, ikiwa kama mwongozo wa maisha Kwa njia hii fasihi simulizi hufunza, huadibu, huonya na kutatua matatizo ya kijamii.

Mambo ambayo tumeyasema hapo juu, yana dhihiril katika ngano ya Kinungu Maria ambayo tunaweza kusema ku imefuata mwelekeo wa jamii na kuwa mwongozo wa maisha katika jamii ya Waswahili. Hivyo maudhui yake yana-ingiliana sana na matarajio ya jamii hii.

Mwanzoni mwa ngano hii tunaonyeshwa mambo kadhaa yanayohusiana na utamaduni wa jamii ya Waswahili Hapa tunaonyeswa kuwa, mtu akifiwa na mkewe hana budi kuoa, akifuata desturi kamili, yaani kuposa na kuoa. Bibi anayeolewa ana wajibu wa kumtunza bwana yake pamoj na mtoto au watoto wa bwana yake ambao wameachwa na mke mwenzake. Jambo la tatu ambalo tunaelezwa kuhusu jamii hii ni kwamba, uzazi ni jambo la majaaliwa. Mtu hujali na mwenyezi Mungu kupata watoto.

Maudhui mengine katika ngano hii yanahusu uhusiano baina ya watu katika jamii. Kutokana na misen katika ngano hii tunaona kuwa uhusiano mwema baina ya watu ni muhimu. Watu wanatarajiwa kusaidiana katika maisha yao ya kila siku. Jambo hili linajitokeza katik maneno ya Kinungu Maria anayesema "leo umenifaa nami kesho nitakufaa, leo imekuwa yangu, kesho itakuwa yako,

na watu ulimwenguni ni kufaana". Kiini cha mambo haya ni kuwa kila binadamu hupatwa na shida ambayo itamfanya ahitaji msaada wa mwenzake. Hivyo tunafundishwa kuwa, ikiwa leo hatuna shida, tujue kwamba kesho itakuja. Yule aliye na shida leo asaidiwe ili naye kesho aweze kusaidia wengine kwani watu ulimwenguni ni kufaana.

Katika ngano hii tunaelezwa udogo wa Kinungu Maria. Lakini licha ya udogo huu, tunamwona akimwambia yule mtoto kuwa akipatwa na shida yoyote alitaje jina lake. Kama binadamu tulivyo, yule mtoto alijisemea moyoni kuwa, "hiki kijinyama kidogo kitanifaa nini?". Hata hivyo tunamwona baadaye Kinungu Maria akimsaidia mtoto huyu. Hili ni fundisho kuwa tusiwadharau wenzetu kwa udogo au umaskini wao na kuwaona kama wasiokuwa na la kutusaidia. Kila mtu katika jamii ana sehemu yake ambayo anaweza kuimudu kulingana na uwezo wake. Pia tunafundishwa kuwa, uwezo wa mtu hauandamani na maumbil Kinungu Maria licha ya udogo wake alikuwa Mfalme wa Wanyama.

Maudhui mengine katika ngano hii, yanahusu dhul na mateso. Tunaelezwa kuwa, yule bibi aliyeolewa, hakumpenda mtoto wake wa kambo. Nia yake kubwa, ilikuw kuondoa uhai wa mtoto huyu. Alimpa mateso mengi sana, hata kule kusumbuka msituni ilikuwa kazi ya bibi huyu Kwa upande wa yule mtoto tunaelezwa kuwa alikuwa mtiifu, na aliendelea kuwa mtiifu. Hapa tunaona kuwa

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

mtoto huyu alilipa mateso hayo kwa kuwa mtiifu na kutendea wengine mema kama vile Kinungu Maria. Fundisho hapa ni kwamba matendo mema daima hulipwa kwa mema. Kwa mfano kama yule mtoto asingemsaidia Kinungu Maria kule msituni naye pia hangeweza kupata usaidizi kutoka kwa Kinungu Maria.

Tunafundishwa kuwa ingawa tuna mateso, ni muhimu pia kuachilia mateso yetu kwa muda na kusaidia wengine. Pamoja na haya, dhana ya utii imehimizwa sana katika ngano hii. Hasa utii kwa wazazi. Wazazi wanaweza kuwa wazazi halisi au wa kambo. Utiifu usichague wakati, yaani mtoto akiona kuwa anatendewa mema na wazazi wake ndipo awatii, bali ni utiifu wa kila wakati na hali. Tunaambiwa kuwa mtoto huyu licha ya mateso aliyopewa na mama yake wa kambo aliendelea kuwa mtiifu.

MTINDO

Katika kushughulikia ujumbe ambao tumeuona hapo mbeleni, msimulizi wa ngano hii ametumia mbinu kadhaa kuisanii na kuisarifu kazi yake.

Ngano hii imeanza kwa mwanzo wa kawaida yaani ule wa kusema, paukwa ... pakawa, na "Hapo kale paliondokea". Wahusika wa ngano hii ni wanyama na wanadamu, lakini nafsi za wanyama ndizo zimetawala. Wanyama hawa wamepewa uwezo wa kutenda na kusema kama wanadamu. Sifa moja ambayo wanyama hawa wamepewa ni uwezo wa kutumia

maneno yenye kunata na kuvuta msikilizaji. Kwa mfano amechagua maneno kama vile "leo umenifaa, Kesho nitakufaa", "leo imekuwa yangu, kesho itakuwa yako, na "watu ulimwenguni ni kufaana". Maneno haya yanatoa uzito fulani ambao humgusa mtu akaona haja ya kumsaidia mwenzake. Hii ndiyo sababu ambayo inatufanya tuseme kuwa msimulizi amekomaa kimawazo, pia ana ukwasi wa lugha.

Ngano hii ina wimbo. Wimbo katika ngano hudha miriwa kutumbuiza na kupumzisha wasikilizaji ambao huwa wamechoka na masimulizi mfululizo. Pia wimbo hushiriki hadhira katika kazi ya kutamba ngano, kwa sababu wakati mwingine hadhira hutakikana kuimba pamoja na msimulizi. Pamoja na hayo imebainika kuwa, fasihi simulizi huungan tanzu zake ili kuendeleza ujumbe wake.

### 2.3.3 MTU NA MKEWE

Ngano ya Mtu na Mkewe ina wahusika ambao ni Wanyama na Wanadamu. Jambo la kustaajabisha ni kuwa wanyama hawa wamezaliwa na mtu na mkewe. Kwa kuwa fasi simulizi au andishi inamhusu binadamu hatuna budi kusem kuwa wanyama walio katika ngano hii wanasimamia binadam

Katika kuchambua ngano tunaanza kwa kusema kuwa mwanzo wa ngano yenyewe unatuonyesha muundo wa jamii ya Waswahili. Tunaona maneno kama vile "Sultan na Waziri". Ingawa maneno haya hayaendelezwi katika ngano, tunaweza kusema kuwa baada ya Waarabu

Kuja Uswahilini, Waswahili waliathiriwa na mfumo wa kisiasa wa Waarabu ambao ulikuwa na Masultan wenye Mawaziri.

Maudhui katika ngano hii ni mengi. Maudhui haya yanaendelezwa na wahusika ambao ni wanyama pamoja na wanadamu. Kwanza tunaona kuwa ngano hii inatufunza juu ya uhusiano baina ya mama na watoto wake. Mama katika ngano hii amezaa watoto saba, sita wa kinyama kama tulivyoambiwa na mmoja ndiye binadamu mwanamke. Baada ya kuwazaa tunaambiwa kuwa watoto hawa walitunzwa hadi wakawa wa kusaidia katika kutekeleza shughuli mbalimbali za nyumbani.

Jambo linaloingiliana na utunzaji wa watoto ni malezi. Ingawa watoto hawa walikuwa wa aina ya kinya wamelelewa vizuri na wazazi wao, ambao hatuwaoini wakinu ngunika juu ya maumbile ya watoto wao. Badala yake wame walea na kuwafundisha kazi hadi wakafikia umri wa kuwa- saidia katika kufanya kazi. Hili ni fundisho kwa wazazi ambao kwa bahati mbaya hupata watoto vilema, vipofu au wenye kasoro za kimaumbile. Wazazi kama hawa wanaambiwa na ngano hii kuwa wana wajibu wa kuwalea watoto wao bila manunguniko yoyote, na watoto hao hawatakosa la kufanya katika jamii.

Maudhui mengine katika ngano hii yanahusu shukr itolewayo na wazazi kwa watoto wao baada ya wao kutenda jambo fulani. Tunaambiwa kuwa ni muhimu shukrani hii itolewe bila upendeleo wowote. Inatakikana itolewe kwa

jumla ambapo kila mtoto atahusishwa ama kila mtoto ashukuriwe binafsi. Jambo la kusifu baadhi ya watoto katika familia moja na kuacha wengine limedhihirishwa hapa kama jambo lenye hatari. Katika ngano hii tunaona kuwa fisi alimuua mama yake kwa sababu alihisi kuwa mama yake hampendi. Kwa njia hii ngano ya Mtu na Mkewe inakuwa onyo kwa akina mama ambao hupenda kusifu na kupendelea mtoto au baadhi ya watoto na kuwaacha wengine Hawa wanaonyeshwa kuwa jambo kama hili halifai. Kule kuuawa kwa yule mama ndiko kunatoa uzito na kuonyesha ubaya wa jambo hili.

Maudhui mengine ni kuhusu tabia mbaya ya mtu kufitini wengine. Katika ngano hii tunaambiwa juu ya mnyama mwingine ambaye aliishi karibu na nyumba ya watoto hawa wa Kinyama. Huyu mnyama kusema kweli alimwo wivu huyu mama mwenye watoto wanaomletea nyama kila siku. Kitu alichokifanya ni kutafuta njia ya kumfitini na watoto wake. Alipo sikiliza wimbo wa yule mama watoto, akasikia kuwa fisi hatajwi katika ule wimbo. Alijua kwamba anaweza kufitini fisi kwa mama yake, hivyo akaamu kuugeuza ule wimbo na kuuimba kwa njia ambayo ingemfanya fisi audhike sana. Baada ya kuugeuza wimbo huo na kuuimba vingine kama ambavyo tumeona katika ngano, fisi alimkasirikia mama yake hata akamkatia maisha. Hivyo tunaona kuwa tabia ya kufitini imejitokeza hapa pamoja na madhara yake. Tabia hii ni mbaya, ndiyo maana watu wengi husema kuwa ni "afadhali mchawi kuliko mwongo mfi

Ingawa tumeonyeshwa kuwa watu wenye tabia ya kufitini wapo katika jamii, tunafundishwa na ngano hii kuwa ni wajibu wetu kuchunguza mambo tunayoambiwa. Lazima tuwe werevu wa kuchunguza mambo kabla ya kufanya uamzi wetu. Werevu kama huu ndio alioukosa fisi. Yeye kwa ujinga wake alifikiri kuwa yule aliyeimba alikuwa mama yake, ndipo aksema,"ah jamani, mimi kila siku naleta nyama kubwa hapa nyumbani, itakuwaje leo mama ananiambia naleta nyama mfu".

Fisi anakuwa mwenye hatia ya kumuua mama yake kwa sababu hakutafiti maneno ya ule wimbo ambao haukuimbwa na mama yake bali na mtu mwingine mwenye nia mbaya. Hili kama tulivyosema hapo mbeleni linasimama kama funzo na onyo kwamba, ingawa kuna waongo wafitini katika jamii, ni wajibu wetu kuyatafiti au kuchunguza maneno yao kabla ya kuyatumia kama ushahidi na utetezi wa kutenda mabaya. Fisi hangemuua mama yake kama angeji patia wakati wa kutafuta ukweli wa mambo yale.

MTINDO

Katika ngano hii tunatazama mbinu alizozitumia msimulizi kuwasilisha ujumbe wake. Msimulizi wa ngano hii ametumia muundo wa masimulizi ambapo ngano hii ni maelezo ya moja kwa moja. Maelezo haya ameyaanza kwa kusema paukwa ... na kuendeleza mwanzo huo na "Hapo zamani za kale ...".

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Pamoja na hayo tunaona kuwa, msimulizi huyu naye ametumia mbinu kadha wa kadha kudhihirisha usanii wake. Mbinu ya kwanza ambayo inajitokeza ni ile ya tashihisi. Kwa kutumia mbinu hii msmulizi amewapa wanyama sifa za kibinadamu, pale anaposema kuwa watoto wakazaliwa wa kinyama, kisha watoto hawa wanazungumza na kutenda mambo sawa na binadamu. Hapa msimulizi anafaulu kutumia wanyama hawa badala ya wanadamu.

Wimbo umetumiwa katika ngano hii, kuendeleza maudhui ya ngano hii. Ni katika wimbo huu, ambapo tunaona maneno yaliyomfanya fisi kukasirika kiasi cha kumuua mama yake. Pamoja na kuendeleza maudhui wimbo huu una uwezo wa kuburudisha na kupumzisha wasikilizaji kutoka kwa maelezo mfululizo. Kwa kufanya hivyo wasikilizaji wanapata nafasi ya kujitayarisha kuendelea kusikiliza maelezo zaidi.

Matumizi ya misemo katika ngano hii ni ushahi kuwa, msimulizi ana ukwasi wa lugha anayoitumia. Kwa mfano kuna msemo kama vile,"mbiu ikipigwa ina jambo". Msemo huu unadhirisha kuwa jamii ya Waswahili hutumia misemo katika maisha yao ya kila siku.

Mwisho katika ngano tunaona mbinu ya litifati pale ambapo msimulizi anatoa nafasi kwa wahusika wake wazungumzie wasikilizaji ingawa ni yeye msimulizi anay ngumza. Mfano hapa ni pale ambapo watoto wengine wana rudi kutoka kuwinda na kupata kuwa mama yao ameuawa. Wanasema wao wenyewe, "leo mama ameuawa".

## 2.4.0 UCHAMBUZI WA NGANO ZA WAKURIA

Baada ya uchambuzi wa ngano za Waswahili, sasa tutachambua ngano za Wakuria zikiwa ni, Mama na Sungura, Wesanganache, na Nyanya na Watoto.

## 2.4.1 MAMA NA SUNGURA

Fasihi simulizi kama ilivyo ina uwezo wa kuona, kutafsiri na kuhakiki maisha ya mtu au watu na mazingira yao katika jamii. Kwa kufanya hivyo fasihi simulizi kama tulivyosema, hututolea picha kamili ya hali halisi ya maisha katika jamii fulani. Ukweli huu wa fasihi simulizi umejitokeza katika ngano hii ambayo tunaichambua.

Katika ngano hii, kuna mambo kadhaa ambayo yanazingatiwa, katika mkutadha wa jamii ya Wakuria. Kwanza tunafahamishwa juu ya kazi muhimu walizozitekelez akina mama katika jamii hii.

Tunaona kuwa kazi za utunzaji watoto, kuteka maji mtoni, kukusanya kuni na kulima mashamba, zilikuwa ni za akina mama. Kazi hizi tunaona kuwa zote zilienda sambamba. Kwa upande wa kutunza watoto tunafahamishwa kwamba ilikuwa muhimu, mama mwenye mtoto mchanga kuwa na mlezi wa kumlea mtoto wakati mama mwenyewe hayupo. Ikiwa ilitokea kuwa mama mwenye mtoto hana mlezi, ilimbi atekeleze shughuli zake akiwa amembeba mtoto huyo ama

amemkalisha chini karibu na mahali pake pa kazi. Pi
miongoni mwa jamii hii, tumeonyeshwa kuwa kulikuwako
wawindaji. Jambo hili tunaliona pale sungura anapos
kuwa, maini yale alikuwa amepewa na wawindaji.

Katika kuzingatia maudhui zaidi, tunaona ku
kuna maudhui yanayotoa mafunzo pamoja na onyo katika
jamii. Katika ngano tunamwona mama akimpoteza mtoto
wake, kwa sababu ya haraka za kukubali na kumchukua
sungura kama mlezi wa mtoto wake. Haraka hii ilitok
na shida kubwa aliyokuwa nayo huyu mama ya kufanya
akiwa na mtoto kila wakati. Linalofundishwa hapa ni
kwamba huyu mama angevumilia au angestahimili mpaka
apate mlezi kutoka mahali panapojulikana. Hivyo ony
ni kwamba, ni hatari kumpa mtu asiyejulikana atokako
kazi ya kumlea mtoto. Hivyo ngano hii inatufundisha
mama walio na watoto wachanga wanahitaji kuvumilia n
kukubali shida ya kuwalea na kuwantunza watoto wao.
Pamoja na hayo wanatakikana kuchunguza tabia na nia
watu wanaokuja kwao na kuomba kazi ya kulea.

Ngano hii ina uzito na umuhimu mkubwa katik
maisha ya siku hizi ambapo akina mama wanahitajika k
kazi mbalimbali na wakati huo huo wawatunze watoto w
Kwa sababu hakuna uwezekano wa kutekeleza kazi hizi
muhimu kutafuta na kumwajiri mtu fulani awe mlezi.
tunajua kwamba siku hizi mtu hasa mama mfanyikazi ha
kuepuka jambo la kumwajiri mtu awe mlezi wa watoto w

tunaonywa kwamba tusimwaajiri mtu yeyote tumpatataye. Mtu huyu anaweza kututendea kama vile sungura alivyomtendea mama mtoto. Sungura alimchinja mtoto na kula maini yake. Labda leo watu walio kama sungura hawatatoa maini ya mtoto ama watoto, lakini kuna hasara nyingi ambazo wanaweza kuzisababisha.

Iwapo mtu ambaye hafahamiki atapewa wajibu wa kuwalea watoto, tunaonywa kwamba asisaminiwe kiasi cha kumwambia baadhi ya siri za nyumbani ama mahali unapoenda na wakati utakaporudi. Mama mtoto alimwambia sungura kuwa anaenda shambani na kuwa atachelewa kurudi. Hili ndilo jambo ambalo lilimfanya sungura apate uhuru na wakati wa kutimiza haja yake, ambayo ndiyo hasa iliyomfanya aitake ile kazi ya kumlea yule mtoto. Ngano hii inatufundisha kuwa, watu kama hawa hawapaswi kuambiwa mahali unapoenda. Asipojua wakati wa kurejea nyumbani huenda atakuwa na woga wa kutenda mabaya kwa sababu hatajua wakati ambao mwenye nyumba atarudi.

MTINDO

Msimulizi ameanza ngano hii kwa kutumia maneno kama vile "Hapo zamani za kale ...". Huu ni mwanzo wa ngano katika jamii nyingi za Ulimwengu. Wahusika wake ni sungura pamoja na wanadamu, lakini anayeingiliana sana na sungura ni mama mtoto. Msimulizi amempa sungura lugha na uwezo wa kutenda mambo kama binadamu. Hivi msanii huyu ametumia mbinu ya tashhisi ili aweze

kuwasiliana na wasikilizaji wake.

Wimbo pia umetumiwa katika ngano hii. Wimbo huu unaendeleza maudhui na vilevile unaburundisha wasikilizaji wa ngano. Maneno ya wimbo huu yanasikitisha sana na yanawafanya wasikilizaji watake kusikiliz ngano zaidi kwa madhumuni ya kutaka kujua kitu kitakach mfikia sungura baada ya kumuua mtoto.

Mbinu nyingine ambayo ameitumia msimulizi ni ile ya litifati. Hapa msimulizi anatufanya tuhisi kuwa si yeye anayeongea bali ni mhusika mwenyewe. Kwa mfano tunamwona sungura akisema, "huyu ni mama gani hana mlezi, kana kwamba hakuna walezi".

Pamoja na hayo yote ambayo tumeyajadili, msimulizi wa ngano hii ameitumia mbinu ya tashbihi. Mbinu hii tunaiona pale ambapo msimulizi anaposema kuwa, sungura alinoa kisu kikawa na makali kama wembe. Katika jamii ya Wakuria wembe inachukuliwa kama mfano wa kitu kilicho na makali ya hali ya juu. Kwa kutumia mbinu hii anatufanya tuhisi vile kisu hicho kilivyo kuwa, hasa kwa upande wa makali yake na ile kazi ambayo kulitakikana kuitekeleza.

Kwa kutumia mbinu hizo chache, ambazo tumezipit msimulizi anafaulu katika kurejesha ujumbe wake na kutoa mafunzo katika jamii yake, kama ambavyo tumeona. Pia anafaulu kutuonyesha kuwa, pamoja na kufunza, fasihi simulizi huburudisha.

## 2.4.2 WESANGANACHE

Maudhui katika ngano hii, yanaweza kugawanyik katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni maudhui ambayo yanatupa picha kamili ya uhusiano baina ya ndug wawili. Ndugu hawa ni kaka na dada yake. Katika jamii ya Wakuria matarajio ya dada kwa kaka yake ni tofauti na yale ambayo ndugu yake wa kiume aliyonayo. Hii ndiyo sababu, tunaonyeshwa katika ngano kuwa, dada yake Wesanganache alipoona kuwa anashida ya mavazi ya binti zake aliwatuma kwa kaka yake, ambaye ndiye mwenye jukumu la kumsaidia dada yake apatwapo na shida ambayo mumewe hawezi kuitatua. Hivi ni kusema kuwa ndugu wa kiume ana wajibu wa kumsaidia ndugu yake wa kike hata baada ya kuolewa.

Jambo la pili ambalo tunaelezwa na ngano hii kuhusu jamii ya Wakuria ni kuwa, mtoto wa kike anahita kuvaa vizuri kila wakati. Mtu ambaye anaweza kumpatia mavazi bila kunungunika ni mjomba wake. Mjomba wake anapotakikana kutoa nguo, anajua kwamba ni lazima ate-keleze jambo hili ipasavyo, ndiyo maana Wesanganache anasema "ni vyema".

Katika sehemu ya pili ya ngano hii tunaona maudhui ambayo yanahusu matarajio ya jamii kwa watoto. Msimulizi wa ngano hii ametumia wasichana wawili kuendeleza maudhui hayo. Pamoja na wasichana hawa

kuna aina tofauti za wanyama ambao tunajua kuwa wanasimamia binadamu. Jambo analoliendeleza msimulizi huyu ni kwamba, heshima, na utii ni vitu viwili vyenye maana katika jamii. Kwa upande mwingine anatuonyesha kuwa dharau na uongo ni sifa mbaya ambazo matokeo yake ni hasara na majuto. Jambo la tatu ni kwamba kuvumili ni jambo muhimu, iwapo mtu anataka kutimiziwa au kutimiza jamba analolitaka.

Katika kuendeleza dhana ya heshima, utii na uvumilivu, msimulizi ametuchorea msichana wa kwanza. Msichana huyu anafuata kila jambo analoambiwa na wanya pamoja na wanadamu. Anapokutana na kibibi mzee tunamwona akimpa heshima na kuyafuata maagizo yake. Anapo fika kwa mjomba wake, anafanya yote kulingana na maagi ya mjomba wake. Kutokana na utiifu wake pamoja na kuvumilia kwake, tunamwona akichochea moto ili apike nyama ziive bila kufunua. Matokeo ni kuwa anapata ngu viatu, shanga na vitu vingi vya thamani na anarudi kwao akiwa mwenye furaha.

Kwa upande mwingine tunaonyeshwa kuwa, kudharau au kupuunza maagizo tunayopewa si jambo la busara. Msichana wa pili ndiye mhusika anayetoa funzo hili. Alipokutana na bibi mzee, hakushughlika na maneno aliyomwambia. Badala yake alifuata maneno yake mwenyewe. Huko kwa mjomba wake, badala ya kufanya yal ambayo ameambiwa kufanya, anafanya kinyume. Kwa mfano

yule kibibi mzee alipomwambia kuwa, akifika kwa wesanganache asifuate njia nzuri, bali afuate njia yenye samadi, hili analipunza na kufuata njia nzuri. Pili mjomba wake anapomwambia aende kulala kwenye zizi la ng'ombe anarudi kulala ndani ya nyumba. Anapoulizwa ng'ombe gani aliyemkanyaga, anadanganya kwa kuchagua ndume yule mkubwa zaidi. Anaendelea kufanya kinyume cha mambo anayoambiwa hadi anafunua mapipa ya nyama jambo ambalo alikatazwa. Matokeo ni kuwa anakosa nguo, viatu, shango na vitu vingine alivyopata dada yake. Msichana huyu anarudi kwao akiwa mwenye huzuni na majuto.

Maudhui ya ngano hii ni muhimu katika jamii ya sasa, kwa sababu, kila mahali heshima, utiifu na uvumilifu ni mambo ambayo yanahimizwa, nyumbani, mashu kwenye vyuo na mahali popote wanadamu walipo ili wadumi uhusiano mwema.

MTINDO

Ngano hii imeanza kwa maneno "Hapo zamani za kale". Kwa kuiendeleza, msimulizi ametumia mtindo wa masimulizi ya moja kwa moja.

Katika ngano hii kuna matumizi ya tamathali ya tashhisi. Hapa wanyama kama vile fisi na kima, wam pewa uwezo wa kibinadamu hasa wanapozungumza kama wanadamu.

Ngano hii ni ndefu kuliko nyingine mbili ambazo tumezichambua. Hili ni jambo linaloingiliana na mtindo, kwa sababu ngano hii haina misemo wala methali zozote. Msimulizi anaeleza kila jambo wazi-wazi.

Kuna wimbo ambao umebeba maneno yenye mafunzo.. Hili ni jambo la kuonyesha ubingwa wa msanii kwa sababu anatoa ujumbe wake kwa njia nyingi kwa madhumuni ya kuepuka kuchosha wasikilizaji wake. Pia kwa kutumia wimbo huu anaburudisha wasikilizaji wake na hapo hapo anawafundisha. Mbinu nyingine ambay ameitumia msimulizi ni ile ya litifati. Hapa msimul anawapa wahusika wake nafasi ya kuzungumza kupitia k mwenyewe. Kwa mfano, kima alisema "wewe msichana ba yako anaitwa nani?. Tashibi pia ni mbinu ambayo ame tumia msmulizi wa ngano hii.

2.4.3 NYANYA NA WATOTO

Fasihi simulizi ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Watu ndio wanaozalisha utamaduni wao na wao ndio wenye haki ya kuufurahia. Jambo hili limethibi tishwa katika ngano hii ya Nyanya na watoto.

Ngano hii ina lengo la kutoa sababu ambayo inawafanya Wakuria wasitumie nyama ya ndovu ambayo k jamii nyingine hutumiwa. Hili ni jambo la kitamadun na mtu atendaye kinyume yaani kula nyama ya ndovu

huchukuliwa kuwa mwenye hatia kwa sababu anavunja mwiko katika jamii yake. Tunaambiwa kuwa ndovu ni nyanya ya Wakuria ambaye hapo zamani alijigeuza na kukimbilia vichakani.

Katika ngano hii tunaona vile fasihi simulizi hutumika katika kuendeleza imani na itikadi kutoka kizazi kimoja had kingine. Pia tunaona kuwa fasihi simulizi inatoa maelezo au majibu kwa maswali kama vile kwa nini kitu fulani kilitendeka namna fulani na kwa nini wanajamii wanakubali tukio kama hilo.

Watoto wanapowauliza wazazi wao sababu ya kutokula nyama ya ndovu, badala ya kuwaambia kuwa ndovu ni nyanya yao au kutoa sababu nyingine, wazazi au watu wengine wazima, huwajibu swali lao kwa urahizi, kwa kuwatolea ngano hii ambayo bila shaka huwaondolea mashaka yote kuhusu uhusiano wao na ndovu. Ujumbe huu ndio anaodhamiria kuuwasilisha katika jamii, hasa kwa watoto ambao wanatakikana kujua matarajio ya jamii yao.

<u>MTINDO</u>

Ngano hii imeanza kwa maneno ambayo ni ya kawaida katika kutamba ngano. Hivi ni kusema kwamba imeanza kwa maneno ya "Hapo zamani ...". Maneno haya yana umuhimu kwa sababu yanatupa wakati wa matukio ya ngano ingawa umuhimu huo hauwekewi mipaka kwani matukio ya wakati huo yanaweza kutufaa hivi sasa.

Katika kuendeleza maudhui ya ngano, msimulizi ametumia maneno ya kawaida. Anatumia mtindo wa masimulizi ya moja kwa moja bila kutumia msamiati wala methali. Pamoja na haya amejaribu kutumia tamathali za semi hapa na pale.

Msimulizi ametumia mbinu ya litifati. Katika ngano hii tunamwona baba watoto akisema "ah watoto, tangu lini mama yangu akawa zimwi? nitakuja niwachape pamoja na mama yenu kama ndiye amewaambia hivyo". Katika maneno ya baba watoto kuna sauti "ah", sauti hii inatumiwa na mtu ambaye ameshangazwa na jambo fulani Huu pia ni ufundi kwa kuwa msimulizi anafaulu kuonyesha mshangao huo kwa kutumia sauti kama "ah!".

Mbinu nyingine anayoitumia msimulizi huyu kuwasilisha ujumbe wake ni ile ya taswira. Mbinu hii injitokeza pale ambapo msimulizi anasema kuwa, yule mama mkongwe alianza kufura pole pole had akawa kiumbe kikubwa sana chenye kutisha. Taswira ina maana ya picha hivyo tunapewa picha ya kitu kinachofura polepole kama vile unga wa mkate unavyofura polepole na kufikia kiwango kinachotakikana.

## 2.5 TANBIHI

1. Khamis, S.A. (1983) "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Kitanzania". Makala katika Mulika No. 15. Jarida la Taasisi ya Uchunguz wa Kiswahili chuo kikuu, Dar es Salaam.

2. Mohamed, S.A. (1981) "Fani na Maudhui" Makala katik Misingi ya Nadharia ya Fasihi. Kimetolewa na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar.

3. Abdilatif Abdalla, (1980). "Maudhui na Mtindo" Makala katika Zinduko. Jarida la chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

4. Fischer, E. (1959 The Necessity of Art. Penguin Books.

# SURA YA TATU

## 3.0 ULINGANISHI WA MAUDHUI NA MTINDO

### 3.1 UTANGULIZI

Baada ya kuchambua maudhui na mtindo bai ya ngano za Waswahili na Wakuria, tunataka kulinga maudhui hayo pamoja na mtindo uliotumiwa kuyaende maudhui hayo. Kama tulivyosema hapo mbeleni, uling nishi huu ni muhimu katika tasnifu hii kwa sababu, fasihi simulizi kama fasihi andishi ni kioo ambach hutupa picha kamili ya hali halisi katika jamii fu Uhalisi huu ni maisha ya kila siku. Hivyo fasihi hutuonyesha mahusiano ya watu katika jamii, na muh haya yaweza kuwa ya kijamii, kisiasa au kiuchumi. Ulinganishi wa maudhui na mtindo wa ngano ambazo chambua unaweza kutubainishia tofauti iliyoko bain ya jamii ya Waswahili na Wakuria, pamoja na kufana kwa hizi jamii.

Kwa upande wa mtindo tutalinganisha matu na uteuzi wa maneno yanayotumiwa katika kutamba ng Katika ulinganishi huu, tunaweza kusema kuwa tunali nisha ujuzi wa wasimulizi wa ngano hizi zaidi kuli kusema kuwa tunalinganisha mtindo wa ngano zenyewe

Ulinganishi huu umegawanyika katika sehe mbili. Sehemu ya kwanza, inazingatia kufanana kwa maudhui na mtindo baina ya ngano za jamii ambazo t zitaja. Sehemu ya pili inazingatia tofauti iliyok

katika maudhui na mtindo baina ya ngano ambazo tumezichambua.

## 3.2 KUFANANA KWA MAUDHUI NA MTINDO

Fasihi simulizi kama zao na amana ya jamii ina umuhimu na wajibu katika jamii. Katika muktadha wa kuwa na wajibu, tunaona kuwa, fasihi humtazama binadamu na mahusiano yake na binadamu wenzake pamoja na viumbe wengine. Pia fasihi humtazama binadamu na mazingira yake na humtazamisha mazingira hayo ili ayaone.

Ukweli wa jambo hili umejitokeza katika uchambuzi wetu ambao tumeufanya katika sura ya pili. Katika sura hiyo tumechambua maudhui ya ngano sita, tatu kutoka jamii ya Waswahili na nyingine tatu kutoka jamii ya Wakuria. Ingawa jamii hizi zinatofautiana kijiografia, katika kazi hii tutaonyesha kuwa mtindo na maudhui ya ngano hizi yanafanana kwa kiasi kikubwa.

Katika jamii ya Waswahili na Wakuria, tunaona kuwa, ngano zilitumiwa kueleza matarajio ya jamii. Matarajio haya yaliweza kuwa ya kiuchumi, kijamii au kisiasa. Hivyo tunaona kuwa fasihi simulizi, ilitarajiwa kutoa mwongozo wa tabia njema na mahusiano bora baina ya watu katika jamii. Imebainika kuwa, kufanana kwa maudhui ya ngano hizi, kunatokana na matarajio haya ya fasihi simulizi ambayo yanafanana katika jamii hizi mbili.

Maudhui ya kwanza ambayo yanafanana katika ngano hizi, ni yale ambayo, yanatufahamisha shughuli za wakati fulani katika jamii hizi. Maudhui haya tun kusema kuwa, yanatuchorea muundo wa jamii hizi, yakituonyesha njia za kuzalisha mali. Kwa mfano ngan za Waswahili ambazo ni Sungura na Fisi, Kinungu Mari na Mtu na Mkewe, zinatuonyesha baadhi ya shughuli za Waswahili wa hapo zamani. Shughuli hizi ni kama vile kulima, kuchunga ng'ombe, kuteka maji kisimani, kuvua samaki, kuwinda, kukusanya kuni pamoja na kuchanja kuni. Pia tunaonyeshwa kuwa hapo zamani, Waswahili walipanda mimea kam vile migomba. Katika kutekeleza shughuli hizi, binadamu walikuwa na maingiliano mbali mbali.

Maudhui kama haya ya ngano za Waswahili ni sawa na haya ambayo yanajitokeza katika ngano za Wakuria. Ngano kama vile, Mama na Sungura, Wesangana na Nyanya na Watoto, zinatuonyesha baadhi ya shughuli walizo kuwa nazo Wakuria wakati huo. Shughuli hizi zilikuwa kulima, kuteka maji, kukusanya kuni na kuwin

Katika jamii ya Waswahili na Wakuria ngano zilitumiwa kufundisha. Mafunzo yaliyotolewa kupitia kwa ngano yalikuwa ya aina tofauti. Kwa mfano kuliku na mafunzo juu ya mila na utamaduni, imani na itikadi za jamii na mengine mengi. Maudhui yanayofundisha juu ya imani na itikadi, mila na utamaduni yanapatikana

katika ngano za jamii hizi mbili. Ngano ya Kinungu Maria, inaendeleza dhana ya majaaliwa. Waswahili wanaamini kuwa, maisha ya mtu hutegemea bahati yake, iwe nzuri au mbaya. Bahati hii ndiyo humwongoza kupata mazuri au mabaya. Hivyo binadamu anapaswa kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kila jambo. Pia ngano hii inaendeleza desturi za Waswahili zinazoingiliana na ndoa.

Ngano ya Wakuria, Nyanya na Watoto ina maudhui yanayofanana na yale ya Kinungu Maria. Ngano hii inaendeleza imani na itikadi za kijamii. Katika mila na desturi, imani na itikadi za Wakuria, ndovu ni mnyama ambaye ana uhusiano wa karibu sana na watu. Uhusiano huu, sio ule wa kushiriki pamoja na watu katika kutenda mambo fulani, bali ni uhusiano wa imani kwamba hapo zamani, ndovu alikuwa ni nyanya yao aliyejigeuza na kuwa ndovu kisha akakimbilia vichakani. Hadi sasa Wakuria hawatumii nyama ya ndovu.

Ngano hii inatumiwa kuendeleza imani hii, kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kama ilivyo kawaida, wanajamii, hawapewi nafasi kuuliza maswali juu ya mambo ya kitamanduni. Lakini linalojulikana ni kwamba, Wakuria hadi sasa ni mwiko kwao kula nyama ya ndovu.

Mahusiano baina ya watu katika jamii, ni jambo ambalo limezingatiwa katika ngano za jamii hi mbili. Mahusiano haya ni ya aina nyingi. Katika kufundisha juu ya mahusiano haya, tunaonywa pia ju ya mambo mbalimbali yanayotokea kukiwa na mahusianc aina fulani. Hivyo katika ngano ya Sungura na Fis tunafundishwa juu ya uhusiano wa Kirafiki pamoja nε hasara zake. Ingawa katika jamii urafiki hudhamini sana, tunaonywa kuwa, si marafiki wote wazuri. Ni wajibu wetu kuchunguza na kupima vilivyo mapendekez ya marafiki wetu. Pia tunafundishwa kuwa haifai kι mzaha kila wakati.

Ngano ya Kinungu Maria, ina maudhui ya uł Kuna uhusiano baina ya mtoto na wazazi hasa wazazi kambo. Pia tunaona uhusiano baina ya mtu na watu ι Kusaidiana, kutii na kuvumilia ni mambo muhimu, yar tokeza katika ngano hii. Ngano ya Mtu na Mkewe, iı juu ya uhusiano pia. Kuna mafunzo kuhusu uhusiano ya mama na watoto wake. Tunatahadharishwa juu ya watı tabia ya kufitini wenzao na kuharibu uhusiano mwemε Katika ngano hii tunaonyeshwa, mambo yanayoleta uhı mwema, na uhusiano mbaya.

Jambo hili la uhusiano baina ya watu kat jamii, kimechukua nafasi kubwa sana katika ngano zε Wakuria, na ndiyo tukasema kuwa, maudhui ya ngano h

yanafanana. Ngano ya Wesanganache, inazungumzia uhusiano baina ya dada na kaka yake, watoto na watu wazima. Ili uhusiano huu uweze kudumishwa, tunaona kuwa, heshima na utii ni mambo muhimu.

Katika kujadili kufanana kwa maudhui baina ya ngano za Waswahili na Wakuria, imebainika kuwa, yanafanana katika viwango vitatu. Katika kiwango cha kwanza, kuna maudhui ambayo yanatueleza shughuli za jamii hizi mbili katika wakati fulani. Ni katika kiwango hiki ambapo tunaonyeshwa muundo wa jamii hizi na mbinu zao za kuzalisha mali. Tunaona kuwa shughuli hizi ambazo ni kama vile, kulima, kukusanya kuni, kuvua samaki, kuteka maji mtoni au kisimani, baadhi yake zinafanana katika jamii hizi mbili.

Katika kiwango cha pili, tumeona kuwa, fasihi simulizi, ilitumiwa, kuwakilisha itikadi za jamii hizi mbili. Ngano ya Kinungu Maria ambayo ni ya Waswahili, inaendeleza dhana ya majaaliwa, pamoja na mila au desturi zinazopaswa kufuatwa mtu atakapo kuoa. Ngano ya Nyanya na Watoto, ambayo ni ya Wakuria, inaendeleza imani na itikadi kuhusu ndovu. Wakuria wanaamini kuwa ndovu ni nyanya yao ambaye hapo zamani alijigeuza na kukimbilia vichakani.

Katika kiwango cha tatu ni maudhui ambayo

yanahusu mafunzo na maonyo mbalimbali katika jamii. Maudhui haya yamejitokeza katika ngano zote ambazo tumezichambua. Kwa mfano, ngano za Waswahili zinatoa mafunzo mbalimbali pamoja na maonyo. Haya yamejadili kwa kirefu katika sura ya pili. Vivyo hivyo ngano za Wakuria ambazo tumezichambua, maudhui yake mengi yana husu mafunzo na kuonya juu ya mambo mbalimbali. Maud haya yanafanana na yale yanayopatikana katika ngano z Waswahili.

Kwa vile tumesema kuwa mtindo katika tasnif hii unamaanisha kunga au mbinu wanazozitumia wasimuli wa jamii hizi. ili waweze kuwasilisha ujumbe wao, tutaangalia zile mbinu ambazo zinafanana baina ya nga hizi.

Jambo la kwanza linalojitokeza hapa, ni kuw wasimulizi wa jamii hizi mbili, wametumia wahusika wa ofanana kuendeleza maudhui ya ngano zao. Ingawa kuna wanyama kama wahusika, tumewahi kusema kuwa, wanyama hawa wanasimamia binadamu na hali yake ya maisha kila siku. Pili tunaona kuwa aina za wanyama ambao wametu kama wahusika zinafanana. Kwa mfano tunaona wanyama kama vile simba, fisi, sungura, ndovu na kadhalika ka ngano za Waswahili. Wanyama kama hawa pia wanapatika katika ngano za Wakuria zaidi katika jambo hili tunac kuwa sungura anapewa sifa ya ujanja katika jamii hizi

Fisi naye katika pande zote anapewa sifa ya upumbavu. Hivyo tunaona kuwa hili ni jambo ambalo limefanana katika ngano za Waswahili na Wakuria.

Wanyama hawa wamepewa uwezo wa kutenda mambo kama wanadamu hasa tukizingatia kuwa sifa moja ya pekee ya binadamu ni lugha. Hivyo wasimulizi wote wametumia mbinu ya tashhisi.

Matumizi ya tashbihi yanapatikana katika ngano za jamii hizi mbili. Tashhihi ni tamathali ambayo hutumiwa kufananisha au kulinganisha vitu viwili kwa kutumia maneno kama vile, mithili, mfano wa, na kama. Tunaambiwa katika ngano ya Sungura na Fisi kuwa, tumbo la fisi lilikuwa limejaa kama gunia. Ngano ya Mama na Sungura ina tashbihi pale ambapo msimulizi anasema kuwa kisu kilikuwa na makali kama wembe.

Wasimulizi kutoka jamii zote mbili wametumia litifati. Pamoja na mbinu nyingine ambazo tumezitaja, tunaona kuwa, wasimulizi wa jamii hizi mbili wametumia wimbo kuendeleza maudhui ya ngano zao.

Matumizi ya sauti kama vile ah!, ala!, "bu!", "ko-ko-ko", yamebainika katika ngano za pande zote. Sauti kama hizi zina umuhimu katika masimulizi, kwa mfano, sauti kama ah! hutuonyesha hali ya kushangaa. Au sauti kama vile "ko-ko-ko" hutufanya tuhisi kuwa

kuna kitu fulani, kilicho gongwa ingawa katika kusimulia ngano msimulizi, hagongi hicho kitu.

Wasimulizi wa pande zote mbili, wametumia m wa maelezo ya moja kwa moja. Maelezo haya yanaanza kwa maneo a ndiyo kwa kawaida, hutumiwa kuanza ngano. Maneno haya ni "Hapo kale ...". au "Hapo zamani za kale".

Taswira imetumiwa na wasimulizi wa ngano za pande zote. Taswira ni picha. Katika ngano tulizozi chambua, tumeona maelezo ambayo yanatupa picha ya hal fulani.

Kutokana na ulinganishi ambao tumefanya, tunaona kuwa ngano za Waswahili na Wakuria zinasimuli kwa njia ambazo zinakaribiana sana. Yaani wasimulizi wa jamii hizi mbili wanatumia mbinu zinazofanana kati kuwasilisha ujumbe wao.

## 3.3 TOFAUTI KATIKA MAUDHUI NA MTINDO

Katika kuzingatia tofauti iliyoko baina ya maudhui na mtindo wa ngano za Waswahili na Wakuria, tunaweza kusema kuwa hakuna mengi yanayojitokeza kujenga ukuta na kuleta tofauti. Kusema kweli, kuna mengi ambayo yanafanana kimaudhui na kimtindo. Kwa kuwa tumewahi kusema ngano za Wakuria na Waswahili zinafanana, kimaudhui na kimtindo kwa kiasi kikubwa, katika sehemu hii tunataka kuona kama kuna tofauti youyote kwa upande wa maudhui na kwa upande wa mtindo

Kimaudhui tunaona kuwa ngano za Waswahili zinatofautiana na za Wakuria pale imani na itikadi za kijamii zinapojitokeza. Jamii ya Waswahili imeathiriwa sana na dini ya Kiislamu, kwa hivyo imani na itikadi zake zinaingiliana sana na dini hii. Kwa upande mwingine, tunaona kuwa, jamii ya Wakuria ingali bado inatawaliwa na mila jadi licha ya dini ya kikristo kuwepo. Hivyo tunaona baadhi ya maudhui ya ngano za Wakuria yanafunza na kuhimiza kuthamini kwa imani na itikadi za jadi ambazo tunaziona katika ngano ya Nyanya na Watoto.

Swala la kutokula nyama ya ndovu si muhimu katika jamii nyingine, lakini miongoni mwa Wakuria linakuwa na uzito na umuhimu. Lazima kuwepo na sababu fulani, ingawa sababu inayotolewa katika ngano si kweli, bado tunaona kuwa ngano hii inakuwa na umuhimu kitamaduni, na ndiyo bado inaendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa upande mwingine, tukifuata muktadha huu, tunaona kuwa, baadhi ya maudhui ya ngano za Waswahili yanahusu dhana ya majaaliwa. Dhana hii imefungamana na dini ya kiislamu. Kwa kuwa dini huingiliana na utamaduni wa jamii fulani, tunaona kuwa dhana ya majaaliwa kama sehemu ya imani na itikadi za jamii ya Waswahili. Dhana ya majaaliwa hufanya watu kuwaamini kuwa

maisha ya mtu huongozwa na bahati. Bahati nzuri au bahati mbaya kwa binadamu ni majaaliwa yake Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo ukipata bahati nzuri shukuru Mungu, na ikiwa bahati yako ni mbaya pia shukuru Mungu. Hii ndiyo sababu tunamwona yule mtoto yatima katika ngano ya Kinungu Maria akiteseka lakini anahimizwa kuwa mtiifu, kwani hiyo ndiyo bahati yake, na bahati ya mtu hutoka kwa Mungu.

Kwa upande wa mtindo, tunaweza kusema kuwa, tofauti imejitokeza sana katika matumizi ya misemo au methali. Ngano za Waswahili zina methali kadhaa, lakin hatuoni methali yoyote katika ngano za Wakuria.

Ingawa katika ngano za Wakuria hakuna methali hatuwezi kusema kuwa katika jamii ya Wakuria hakuna methali. Kuna sababu mbili ambazo zinaweza kutetea usemi huu. Kwanza ni kuwa, Odaga (1984) amewahi kukusanya methali za Wakuria. Hivyo Wakuria wana methali zao. Pili ni kuwa, katika tasnifu hii, tume-chambua ngano tatu peke yake. Hii ni idadi ndogo sana ambayo haitoshi kusimamia ngano za jamii nzima ya Wakuria. Labda huu ulikuwa ni upungufu wa wasimulizi wenyewe kutotumia methali katika ngano zao, au methali katika jamii ya Wakuria hujisimamia zenyewe, yaani hutumiwa katika muktadha tofauti na ule wa ngano. Hata hivyo hili ni jambo ambalo la hitaji utafiti.

Katika muktadha wa tasnifu hii, kutotumiwa kwa methali katika ngano za Wakuria, kumekuwa ni tofauti ya kimtindo baina ya ngano za Waswahili na Wakuria.

## 3.4. HITIMISHO

Katika tasnifu hii, uchambuzi wetu, umetubai-nishia mambo kadhaa, kuhusu fasihi simulizi.

Tumeona kuwa fasihi simulizi ilikuwa na male ya kutoa mwongozo wa tabia njema, mahusiano bora baina ya watu katika jamii, pamoja na kufunza mambo mengi kama vile umuhimu wa mila na utamaduni wa jamii, busar uadilifu, uvumilivu, heshima na mengine mengi ambayo yalitakikana kwa sababu ya kuboresha jamii.

Ni kutokana na malengo hayo ya fasihi simuli ambapo tunaona kuwa, ngano ambazo tumezichambua zina maudhui yenye kufunza juu ya mila na utamaduni, mahusiano baina ya watu, pamoja na kutoa maonyo mbali-mbali ili kutahadharisha watu waepukane na shida mbali-mbali. Pia imedhihirika kuwa, maudhui ya ngano ambazo tumezichambua, yalioana na kuwiana na utamaduni na mfu mzima wa maisha ya jamii ya Waswahili na Wakuria.

Jambo jingine ambalo limebainika ni kuwa, fasihi simulizi iliwatazamisha wanajamii mazingira yao katika ngano za Waswahili na Wakuria tunaona baadhi ya kazi ambazo zilijenga uti wa mgongo wa uzalishaji mali Hili ni thibitisho kuwa, fasihi simulizi ilitumiwa kuendeleza nyenzo za uzalishaji mali. Kazi kama vile kulima, kuvua samaki, kuteka maji an kukusanya kuni,

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

zilifundishwa kupitia kwa ngano ambazo ni sehemu moja-wapo ya fasihi simulizi.

Kwa upande wa mtindo, kuna mambo kadhaa ambayo yamebainika. Jambo la kwanza ni kuwa, fasihi simulizi ni sanaa kama zilivyo sanaa nyingine. Tumeona kuwa ngano zikiwa utanzu mmoja wa fasihi simulizi, zinahitaji usanii wa hali ya juu, ikiwa ujumbe uliomo utawasilishwa. Imebainika kuwa wasimulizi wa ngano, hufanya kazi ambayo imegawanyika katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza kuna kazi ya ubunaji. Sehemu ya pili in kazi ya kufanya ubunaji uwe na uwiano na uyakinifu wa hali halisi ya jamii. Katika kuthibiti kazi hii, fasihi simulizi inakuwa sanaa. Katika sanaa hii maneno ya mdomoni yanakuwa ni muhimu sana.

Ili kuthibitisha usanii wao, tumeona kuwa, wasimulizi wa jamii hizi mbili wametumia mbinu mbali-mbali ili kuwasilisha ujumbe wao. Mbinu hizi zinaing-iliana sana na matumizi ya lugha, pamoja na uteuzi wa msamiati. Katika ngano hizi tumeona vile wasimulizi wanasawiri wahusika, ambao ni wanyama na wanadamu. Wanyama wanapewa sifa fulani ili waweze kutekeleza kazi wanazopewa katika ngano. Kwa mfano, katika ngano, tunaona wanyama wakizungumza na kutenda kazi mbalimbali. Wanyama hawa kama tulivyosema, wanasimamia matendo na tabia za wanadamu.

Kwa kuwa mada ya tasnifu hii ni uchambuzi linganishi wa maudhui na mtindo baina ya ngano za Waswahili na Wakuria, kuna mambo kadhaa ambayo yamel inika.

Jambo la kwanza ambalo limejitokeza katik uchambuzi wetu ni kuwa, ngano za jamii hizi mbili z shabihiana kimaudhui na kimtindo. Sababu ya kushab hiana huku kuyatokana na wajibu wa fasihi simulizi kwa jumla. Fasihi simulizi kama tulivyosema ni zao na amana ya jamii ambayo hushughulikia taratibu maa za jamii. Taratibu hizi ni kama vile mahusiano bai ya watu katika jamii, shughuli za kijamii, kisiasa kiuchumi.

Kwa njia hii imebainika kuwa, fasihi simu ni chombo cha mawasiliano ya hisia za jamii ambazo zitaja. Ngano za Waswahili na Wakuria zikiwa kama utanzu mmoja wa fasihi simulizi, zimetuonyesha vile jamii hizi, zilivyohisi mazingira pamoja na mataraj yake.

Pia tumeona kuwa fasihi simulizi ilifunza bado infunza juu ya umuhimu wa mila na utamaduni wa busara, uadilifu na mengine mengi yenye kuleta maen na amani katika jamii. Utamaduni, busara, uadilifu, ukarimu, uaminifu na mengine mengi ni mambo muhimu kila binadamu. Kwa hivyo katika hali ya ubinadamu

Waswahili na Wakuria ni sawa hasa tukizingatia kuwa jamii hizi mbili ni za asili ya Kibantu. Kwa njia h dhana zao kuhusu uhusiano mwema, tabia njema na maad zinaelekea kuwa sawa. Tofauti inayojitokeza baina y ngano za jamii hizi imejikita kwenye athari za kidin hasa dini ya Kiislamu ambayo imeletwa na Waarabu. Tofauti hii si kubwa sana, labda kungekuwa na tofaut kubwa, kama tungewauliza wasimulizi, wasimulie juu y jambo fulani. Hatukufanya hivyo kulingana na maleng ya tasnifu hii.

Jambo jingine ambalo limebainika katika tasnifu hii ni kuwa, fasihi simulizi ni sanaa ambayo daima iko hai na kuwa hugeuka kadiri historia ya jam inayoizaa inavyogeuka. Katika kugeuka huku, fasihi simulizi inakidhi haja na mabadiliko ya mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Ngano tulizozichambua zimedhihirisha ukweli huo kuhusu fasihi simulizi.

Fasihi simulizi ilikuwa na umuhimu hapo zamani. Hili ni dai la watu wengi hivi sasa. Kutok na utafiti wetu, imebainika kuwa, fasihi simulizi ina umuhimu katika jamii ya kisasa. Katika tasnifu hii tumeona kuwa, fasihi simulizi inaweza kutumiwa kufundisha, kuonya na kutatulia matatizo mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

## 3.5 AMBATISHO

### NGANO ZA WASWAHILI

### SUNGURA NA FISI

Paukwa ... Pakawa,

Hapo zamani za kale palikuwako Sungura na fisi. Sungura na fisi walikuwa marafiki wa chanda na pete. Siku moja sungura akamwambia fisi "rafiki yangu tulime masamba kwani sasa tunaona mwaka unaenda kwisha. Mimi nitapanda migomba na wewe upande chummvi".

Basi sungura na fisi wakaanza kulima mashamba yao. Wakalima hata yakaisha. Hata yalipokwisha, sung akapanda migomba na fisi akapanda chumvi. Kazi ya kupanda ilipokwisha wakakaa kungojea mimea yao. Migom ya sungura ikaanza kukua polepole, lakini chumvi ya fi ilikuwa haijatokeza.

Fisi alipoona hivyo akamwambia sungura, "ah! sungura, mbona wewe migomba yako inakua lakini mimi chumvi yangu hata haijatokeza?". Sungura naye akamwam fisi, "unajua chumvi hukawia sana kumea". Basi fisi akaacha kuuliza hadi alipoona migomba ya sungura imewe ndizi akasema "huyu sungura amenifanya mpumbavu".

Sungura na fisi wakakaa hadi ndizi zikaiva. Fisi akamwambia sungura "haya mimi sasa nitapanda juu ya mgomba nikate vidole vya ndizi nikakuteremshie

sungura akasema haya panda". Fisi akapanda kwenye mgomba. Alipofika huko juu akakata kidole cha kwanza cha ndizi akala, akashika cha pili. Sungura alipoona vile akasema "ah mzee fisi tangu upande juu, unakula ndizi tu hata mimi mwenyewe hunitupii?". Fisi akamwambia sungura "werevu mwingi". Sungura pale pale akajua kuwa fisi ametambua kuwa alimfanya mpumbavu kumwambia apande chumvi na yeye apande migomba. Sungura mara moja akakimbia hadi kwake akatengeneza uta, akarudi pale kwenye migomba. Alipokuja alimkuta fisi ameteremka chini ameshiba kwelikweli, tumbo lake limefaa kama gunia. Basi palepale sungura akavuruta uta wake na kuachilia mshale kwenye tumbo la fisi bu!, fisi akaanguka pale pale akafa. Sungura akachukua kisu chake akamchinja, akatoa kichwa chake, akakiosha vizuri akakifanya kata.

Sungura akaenda akakutana na watu kisimani wakiteka maji bila kata. Badala yake walikuwa wakitumbkiza nguo kisimani kisha wanavuta na kukamlia yale maji kwenye ndoo zao. Sungura alipoona hivyo akawaambia "chukueni kata hii mtekee maji". Basi wakachukua ile kata wakateka maji wakajaza ndoo zao, lakini kata ile ikakatika mtu wa mwisho alipokuwa akimaliza kuteka maji. Sungura akasema "mtanilipa". Mtanilipa kata yangu Kata yangu nilipewa na mzee fisi,"mzee fisi alinilia ndizi zangu". Basi wale watu wakampa nguo

Sungura akachukua nguo yake akaendelea na safari yake. Akaenda, akaenda hadi akafika mahali fulani, akawaona watu wanaanika dagaa, lakini hawana kitu cha kuanikia hizo dagaa. Sungura akawaambia "chukueni ngu yangu hii, mwanikie dagaa zenu. Waka-chukua, lakini nguo ikararuka. Sungura alipoona hivyo akaanza kusema "Mmenirarulia nguo yangu, mtanilipa. Nguo yangu nilipewa na wateka maji, wateka maji, walin katia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu".

Wale watu wakachukua kidagaa wakampa. Akae na safari yake hadi akafika mahali akakutana na mwewe akila mabuu. Sungura akamwambia "chukua kidagaa hiki changu ule badala ya kula mabuu." Mwewe akakichukua kidagaa akala. Sungura alipoona hivyo akaanza kumfuat mwewe na kumwambia "utanilipa kidagaa changu, kidagaa changu nilipewa na waanika dagaa, waanika dagaa walinirarulia nguo yangu, nguo yangu nilipewa na watek maji, wateka maji walinikatia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu" Basi mwewe akatoa unyoya wake akampa sungura.

Sungura akaenda akafika mahali fulani, akakutana na wawindaji wakitengeneza maonza lakini haw manyoya. Sungura akawaambia "chukua unyoya wangu huu mtengenezee maonza. Wakauchukua wakatengeneza maonza

wakaenda kuwinda lakini maonza yote yakapotea.

Wawindaji walipokuja, sungura akawaambia "mtanilipa unyoya wangu, unyoya wangu nilipewa na mzee mwewe, mzee mwewe alikula kidagaa changu. Kidagaa changu nilipewa na waanika dagaa, waanika dagaa walinirarulia nguo yangu, nguo yangu nilipewa na wateka maji, wateka maji walinikatia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu" Wale wawindaji wakampa ufito.

Sungura akaenda akakutana na wachungaji wa ngombe, wakichunga bila fimbo, akwaambia "chukueni ufito wangu huu mfanye fimbo ya kuchungia ngombe wenu" Basi wale wachungaji wa ngombe wakauchukua ufito wakaufanya fimbo wakachungia ng'ombe wao, lakini ufito ukavunjika.

Sungura akasema, "mtanilipa ufito wangu, ufito wangu nilipewa na wawindaji, wawindaji walinipotezea unyoya wangu, unyoya wangu, nilipewa na mzee mwewe mzee mwewe alikula kidagaa changu, kidagaa changu nilipewa na waanika dagaa, waanika dagaa walinirarulia nguo yangu, nguo yangu nilipewa na wateka maji, wateka maji walinikatia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu. Wale wachungaji wakampa maziwa.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Sungura akachukua maziwa yake akaendelea na safari yake. Akaenda akafika kwenye njia panda. Pale akashika njia moja. Alipoenda mbele kidogo akaji-kwaa na maziwa yake yote yakamwagika. Alipoangalia vizuri akaona kuwa amejikwaa kwenye kisiki. Basi sungura akaambia kile kisiki "kisiki utanilipa maziwa yangu. Maziwa yangu nilipewa na wachungaji, wachungaji wali-nivunjia ufito wangu, ufito wangu nilipewa na wawindaji, wawindaji walinitupia unyoya wangu, unyoya wangu nilipewa na mzee mwewe, mzee mwewe alikula kidagaa changu, kidagaa changu nilipewa na waanika dagaa, waanika dagaa walinirarulia nguo yangu, nguo yangu nilipewa na wateka maji, wateka maji walinikatia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu". Hapo hapo, sungura akakipiga kile kisiki kwa miguu yake hata akaking'oa akakichukua, akaendelea na safari yake.

Akaenda hata akaona kinyanya kizee. Kinyanya huyu alikuwa akichanja miguu yake aufanye kuni za kupikia kunde zake. Sungura alipoona hivyo akamwambia "chukua kisiki hiki uchanje upate kuni za kupikia kunde zako. Kinyanya akachukua kile kisiki akakichanja kikawa kuni akapikia kunde zake hadi zikaiva. Zilipoiva yule akzichukua akala zote bila kumpa sungura.

Sungura alipoona hivyo akachukua moto akachoma

nyumba ya yule kinyanya naye akiwamo. Kinyanya alipoona moto akasema "Sungura nachomeka". Sungura naye akamjib kwa kusema "kufa umekula kunde mwenyewe na hizo kunde zimeivishwa na kuni zangu, kuni zangu nilipewa na kisiki, kisiki kilinimwagia maziwa yangu, maziwa yangu nilipewa na wachungaji, wachungaji walinivunjia ufito wangu, ufito wangu nilipewa na wawindaji, wawindaji walinitupia unyoya wangu, unyoya wangu nilipewa na mzee mwewe, mzee mwewe alikula kidagaa changu, kidagaa changu nilipewa na waanika dagaa, waanika dagaa walinirarulia nguo yangu, nguo yangu nilipewa na wateka maji, wateka maji walinikatia kata yangu, kata yangu nilipewa na mzee fisi, mzee fisi alinilia ndizi zangu". Sungura akakimbia akaenda zake.

Ngano yangu ikomee hapo.

KINUNGU MARIA

Paukwa ... Pakawa.

Hapo zamani paliondokea bwana mmoja. Bwana huyu alikuwa na mke. Huyu mke akamzalia mwana kisha akafariki dunia. Basi yule bwana akakaa, akaona ni her atafute mke mwingine ambaye atamfaa pamoja na mtoto wake. Basi akatafuta mke, akaposa akaoa. Yule bibi akaja naye Mungu akamjaalia akapata mtoto vile vile.

Alipopata mtoto wake, akampenda sana, lakini yule mtoto wa marehemu mke mwenziwe akamchukia sana,

akawa anamtendea mambo mengi maovu. Huyu bibi akawa anamtafutia njia za kumuua. Akafikiria kwa muda mrefu ndipo akaona njia. Akasema, "kule msitu kuna wanyama wengi wa kali sana ambao wakimpata wat maliza haraka sana. Basi akawa kila siku anamtuma huko msituni akatarajia kuwa yule mtoto akutane na mnyama mbaya amdhuru. Bibi huyu alikuwa anabaki ny na mtoto wake ambaye hakutaka afanye kitu chochote. Yule mtoto wa kambo, licha ya mateso aliendelea kuw mtiifu, wala hakuna siku aliyokataa kwenda kutafuta kuni.

Kule msituni kulikuwa na wanyama wa aina Sasa ikawa kule msituni wanyama walikuwa na mfalme Mfalme wakati huu alikuwa kijinyama kidogo kiitwach Kinungu Maria. Siku zote Kinungu Maria alipokuwa a kwenda kutembea alifuatana na wanyama wengine amba walikuwa mawaziri na maasikari wake.

Siku moja Kinungu Maria akaona ni afadhal atoke mwenyewe aende kudadisi vile hali ilivyo. Ak sana asijulikane. Lakini hata hivyo wanyama wengir ambao walimwonea wivu walikuwa wamemwona. Wanyama walikuwa maadui wake. Basi alipotoka siku hiyo, al peke yake bila maaskari wake. Alipoenda mbali kido kwake, alikutana na maadui wake, nao wakaanza kumpi Mara tu akatokeza yule mtoto akienda kutafuta kuni.

Yule mtoto alipoangalia vizuri akaona wanyama wakubwa wakipigana na kijinyama kidogo sana. Hapo hapo yule mtoto akaona kuwa huku kulikuwa kuonea kwa hali ya juu akaamua kumsaidia Kinungu Maria.

Baada ya vita, wale wanyama wakakimbia, Kinungu Maria akamshukuru yule mtoto, akamwambia "leo umenifaa, nami kesho nitakufaa, leo imekuwa yangu, kesho itakuwa yako, na watu ulimwenguni ni kufaana. Ukipatikana na shida wakati wawote kwenye msitu huu, basi liite jina langu". Yule mtoto akajisemea moyoni, " "Kijinyama kidogo hivi kitanifaa nini?". Yule mtoto akaen( kutafuta kuni na kisha akaenda kwao. Akaendelea kuwa mtiifu atumwalo hulitenda hata kama ni la mateso.

Siku nyingine tena akatumwa kuni kule kule msituni. Safari hizi zote mamake wa kambo akimtakia mabaya yampate. Siku hiyo akaenda akapotea njia kabisa. Akasema "Sasa nyumbani sikupati na hapa nilipo kuna wanyama wakali natafanya nini? Akafikiri kwa muda kisha akasema, "ah wacha nipande juu ya mti huu mrefu nilale." Basi akapanda juu ya mti akalala hadi asubuhi. Asubuhi alipotaka kuteremka, lo! akaona simba mkubwa chini ya ule mti. Ikawa sasa yule mtoto hana la kufanya. Kumbe kule chini ya mti kulikuwa na kidimbwi cha maji ambapo wanyama walikuja kunywa maji. Simba alipoondoka, wanyam wengine pia walikuja kunywa maji. Walipofika pale, wakaona kivuli cha yule mtoto kwenye maji, wakasema

"ah jamani hapa pana mtu, lakini wakitazama juu hawamwoni huyo mtoto. Lakini yule mtoto akaanza kuimba hi

Ndimi mtu ndimi nyama
Kinungu Maria

Wanyama wakazidi kuja pale kunywa maji na wote wakifika wanasema "pana mtu hapa. Na yule mtoto akaim wimbo wake akisema;

Ndimi mtu ndimi nyama
Kinungu Maria

Ikaendelea hivi hadi mawaziri wa Kinungu Maria wakaja kunywa maji. Wanyama wengine wakasema "pana mtu, pana mtu" na yule mtoto akajibu kwa wimbo akasema

Ndimi mtu ndimi nyama
Kinungu Maria

Wale mawaziri waliposikia jina la Kinungu Maria, wakas "ala mbona ataja jina la Mfalme wetu?, labda yuko hata Wale mawaziri wakakimbia hadi kwa Kinungu Maria, wakamw mbia kuwa, kuna kivuli cha mwanadamu kisimani, naye akiulizwa ajitambulishe anataja jina lako. Ndiyo maan tumeona tuje tukwambie.

Basi mfalme Kinungu Maria akachukua jeshi la wakaenda hadi pale alipokuwa yule mtoto. Walipofika pale wakasema "Kuna mtu, kuna mtu", Yule mtoto naye akajibu kwa ule wimbo wake akasema;

Ndimi mtu ndimi nyama
Kinungu Maria.

Kinungu Maria aliposikia hivyo akapanda juu mtini. Alipofika huko akamwona yule mtoto akamwambia "leo imekuwa siku yangu ya kukulipa wema wako ulionitendea siku ile". Kinungu Maria na jeshi lake wakampeleka yule mtoto hadi mjini akaenda nyumbani kwao na kuni zake salama salimin.

Ngano ikomee hapo

MTU NA MKEWE

Paukwa ... pakawa,

Hapo kale palikuwako na Sultan na Waziri na watu wote walikaa kukaa kwa furaha na buraha. Bwana mmoja na mkewe walikaa, hata siku moja Mungu akawajaalia kizazi wakazaa wana wao saba. Lakini wana hao sita walikuwa wa kinyama. Mmoja tu ndiye alikuwa binadamu mwanamke. Wale watoto wa Kinyama walikuwa simba, chui, ndovu, nyati gude na fisi.

Huyo bwana na mkewe wakawatunza watoto wao hadi wakawa wakubwa wakutunwa kwenda kufanya shughuli mbalimbali. Wale watoto wa kinyama wakawa wanaenda mwituni kutafuta nyama. Kila walipoenda, fisi alikuja na nyama kubwa kuliko wenzake. Waliporudi kutoka msituni na kufika nyumbani, gude alitangulia na kusema, gugu,gugu, gugu, na mama yao alitoka kuja kuwalaki akiimba hivi.

Chihuhu vuka kombe aha! x 2
Simba baba, chui baba, simba baba
nzo kuno na mbogazo aha.

Ikawa kila siku wakienda na kurudi, mama yao huwakaribisha nyumbani kwa wimbo huo. Lakini karibu na nyumba yao, kulikuwa na mnyama mwingine ambaye kila akisikiliza wimbo wa yule mama, hasikii jina la fisi likitajwa na ilhali yeye ndiye alilete pande kubwa la nyama. Basi huyu mnyama akaanza kuiga ule wimbo kivyake akimdunisha fisi yeye aliimba hivi;

Chihuihui vuka kombe aha! x 2
Simba baba, Chui baba, Simba baba
nzo kuno na mfuzo aha

Basi yule mtoto wa aina ya fisi aliposikia hivyo aliudhika sana. Akasema "ah jamani mimi kila siku naleta nyama kubwa hapa nyumbani, itakuwaje leo mama ananiambia ninaleta nyama mfu". Fisi akamwekea mama yake fitina. Keshoye, fisi akajitia kuumwa, akasema "mama mimi leo siendi kutafuta nyama, nina homa mbaya sana". Wale ndugu zake wakaenda kutafuta nyama msituni kama kawaida yao.

Mama yao akawa anamshughulikia fisi kwa sababu ya ugonjwa wake. Akapuliza moto, akabandika sufuria la uji, baada ya uji akaweka wali, vyote hivi kwa ajili ya mwanae mgonjwa. Alipomaliza akamwekea fisi

uji kwenye kikombe akampelekea. Fisi akashika kikombe cha kwanza, akanywa akamaliza, cha pili pia akanywa akamaliza, cha tatu hakukishika bali alimrukia mama yake na kumkatakata vipande ambavyo alitupa huku na huku. Alipomaliza kuua mama yake akarudi kitandani akaanza kutetemeka ili kuonyesha alivyo mgonjwa.

Ndugu zake waliporudi walianza kusema Mmia, Mmia, Mmia, lakini mama yao hakutokeza kuja kuwalaki. Wakasema "yuko wapi mama yetu?, leo ameuliw mbona haji kutulaki wala kutuimbia?".

Wakaenda haraka ndani ya nyumba yao, kufika ndani lo! wakakuta vipande vya mwili wa mama yao vimetapakaa kila mahali.

Fisi naye pale kitandani alikuwa nakema eh, eh, ili kuonyesha alivyo mgonjwa. Wenzake wakamuuliza, "fisi ni nani amemua mama?" fisi akanyamaza t Wakamwambia "fisi ni wewe tu umemua mama. Fisi akase "mimi! hamnioni vile nilivyomgonjwa?". Basi wale ndug zake wakasema "tutakula kiapo". Fisi naye akasema na "mnilishe". Basi kesho yake mbiu ikapigwa ko-ko-ko, mbiu ikilia ina jambo. Hii ilikuwa mbiu ya kiapo.

Watu wakaja, wakachimba shimo refu sana. Baada ya kuchimba, wakafunga kamba nyembamba kwenye mi miwili, mmoja huku na mwingine kule, katikati kukawa n lile shimo. Wakasema kila mmoja atapita akitembea

kwenye kamba. Aliyeua mama atatumbukia kwenye lile shimo na ambaye hakutenda hicho kitendo atapita salama salimi. Basi simba akaanza, akapita, akaja ndovu akapita, wote wakapita hata yule mtoto wa kike, akabakia fisi. Wakati ukafika wa fisi. Ingawa alikuwa na woga, alianza mwendo juu ya kamba. Akaenda, lakini alipofika kwenye lile shimo alianza kutetemeka na hapo hapo akaanguka na kutumbukia shimoni mbu! akafia humo, na watu wote wakajua kuwa ni yeye aliyeua mama yake.

Wale ndugu zake wengine wakarudi mjini wakamtunza ndugu yao wa kike hata akapata mume akamposa akamwoa.

Ngano yangu ikomee hapo.

NGANO ZA WAKURIA

UMUKUNGU NO OGATOCHO

Karai hayo nkanyora umukungu onde aho, urusiko ronde akaibora omona. Gukugira eno atarenç na moreri, akaya araya no omona wae oyo kera hase. Akagenderia kehayo bene, hano aya ichinkwi aya no omona amogongo, hano aya mogondo gose gesaka hare kuya no omona amogongo.

Oronde akaya mogondo. Mogondo hara akaý no omona, akamwikalia hanze akawansa korema. Hayo hayo ogatocho akaheta mogondo hayo. Hano Ogatocho akomaha kebore omona ora anoora, akagamba iga "on mukungu akwirerera nkanya mbareri babora?" Umukun ora akagamba Iga "Weiya Ogatocho weto tandera mbe.

Ogatocho hano akuigwa Igo, akaigwa buya kemwe, akaya hangi no omona akamwimikia na kowanza komobenera amabina amaiya. Umukungu ora akaigwa b hata we, gukugira anyore omoreri ono araya aratege omona wae hano aya gokora emenemo gee.

Ichinsiko chikaheta ichincharu, ogatoc amenyere kumukungu ora na aragenderia gotegerwa om hano umukungu ora aya ahase nyaborebe. Omona ora akagenderia gukina na kuba omonene.

Oronde Umukungu ora akamuta kuya mogondo agatebia ogatocho iga tarangohe kuringa kohayo niga Ogatocho amahene omona buya kemwe arare atakamshumbura. Hano Umukungu ora asokiri kugamba gayo agatanura kuya mogondo.

Nigo Umukungu ora aibiye igo, Ogatocho agato omona ora hanse akawansa gokoma ichinkwi na kuhuta omoro Hano agosokia agacha akaimikia egekebi akawansa kugitiria. Akagitiria igo gekogena kewembe. Hakumia akaimikia omona ora akamogoga, akamohobura enda, akamsia amani naamara, omobere gonde go akahira kogetanda hakurwa akagubisia buya akagringa gosamba amani na amara gara. Hano gakohea, ogatocho agaikara akarea buya akaigota na gano gatamere, akabekera nyakwabo omona ora.

Hano gukuhika omobaso kimwi, Umukungu ora agacha. Nigo Ogatocho amoroche igo, agekenya kuya harew na kogamba iga, "eh!, eh! rero omona araye, nemwisabiri arure moragiyi, kohayo taranguhe kubokachei". Umukungu ora akahabwa igitumbe isiko no ogatocho, hakurwa ogatoch akamolentera obikima na amani. Umukungu ora akaburia iga "ogatocho nehai urusiri amani gano?" Ogatocho akagamba iga nabaguimi bang'aye. Hano umukungu ora akowansa koragera, ogatocho akawansa kubina iga;

Nyamorea akani ko omona wae

Nyamorea akani ko omona wae

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Umukungu ora akaigwa akaburia, akaburia Ogatocho Iga, "niyeke hayo ukubina?" Ogatocho agakira. Umukungu ora akagenderia koragera. Guiki Ogatocho akawansa kubina aragamba Iga, Nyamorea akani ko omona wae.

Umukungu ora akahatera koragera, akaberekera ogatocho sibono ogatocho akanga gucha, akawansa kuiyereria hangi hayo. Umukungu ora agasoha nyumba akaya boree, hano akuya kogota omona agatokera iga ni risencho reno retana mara hamwi na amani. Umukungu ora akamanya iga amani gara akareye na go omona wae. Nkio ogatocho akabinere Kehara. Akawansa kumgia Ogatocho, hano atora hano, Ogatocho atora ahande. Hano atuna komogota Ogatocho abina Iga;

Ogotere inkurokuro x2

Ogotere inkurokuro x2

Ndache ntebi abagaka

Akarugia Ogatocho igo akanga komogota ronde. Ogatocho akang'osa kuya kamasana agatiga umukungu ora arakura.

<u>WESANGANACHE</u>

Karai hayo nkanyora Omogaka onde aho, arabere-kerwa iga Wesanganache. Omogaka Oyo nkanyora no omome wa kera gento. Wesanganache nkanyora nana musubati omobo ono wanyore atetwa kuya ahase hande aharai na mosacha wae tarenge na binatohei.

Urusiko ronde musubati omobo Wesanganache a( bia mosacha wae iga "Mbuya hano tugatoma umwiseke wet( omonene ono kuya omamai wabo ayi gutuna ichingebo kuigira agoterwa bokong'u". Bagaitaberiana iga umwis( wabo agenede gutuna ichingebo Wesanganache.

Bakaberekera umwiseke wabo oyo bakamotebia hana bagutuna iga agende, hatawe agaitabiria. Nyakwa akamosemiria ibiakorea biakorea gonchera. Urusiko ro hika agatanora kuya omamai wabo. Akawansa kogenda, akagenda igo, akahika kogesaka ekenene agasikana egekondo. Egekondo keno gekamburia iga "mwiseke nowang' ore?" umwiseke ora akagetebia, guiki gekamburia iga "nehai ukuya?"

Ndaburia owesanganache

Nyora atanyite ankore mokari
Niyi ndaruga'ndamoherera

Hano agosokia kubina, egekondo gekamba iga "Ooh, kana kura no Wesanganache ukuya! Maha ench neno oragotere igo uhike aharabu. Umwiseke ora akago amang'ana gara ge egekondo kera, akagenda igo akahik ihumbu yende. Hano akuhika hayo agasikana inyamuru rai eraya kunywa amanche gesaka. Inyamururai ekamubu iga "mwiseke nowang'ui ore?" aka getabia, gukwi pkab iga nehai ukuya? Umwiseke ora akawansa kubina kehara abinere aratebia egekondo hano akuya. Hano inyamurur ikuigwa iga no Wesanganache akuya, ekamotebia iga,

tamaha enchera neyo irakuhiki O Wesanganache.

Umwiseke ora akagenderia norogendo roe kuya omamai wabo, gonchera akaya arasikana ichitinyi na kera tinyi ikaya iramburia hano akuya, nawe akaya arachitebia hano akuya huhetera kuibina ree rera bene.

Akagenda igo, hano agutuna kuhika O Wesanganache agasikana umukungu ono akunguha. Umukungu oyo akamuburia hano akuya, akamtebia iga no Wesanganache akuya Umukungu ora akamworokia omugi go Wesanganache. Akamotebia iga hano akuya ahetere gukihita kera kena orotente, atakahetera gonchera nchiya era.

Umwiseke ora akagenda igo hano akuhika o mamai wabo agakora kehara bene umukungu ora amotebiri. Akagenda korotente igo akahika isiko akawansa kubina guiki,

Ndaburia O Wesanganache
Nyora atanyite ankore mokari
Niyi ndaruga ndamoherera

Hano Wesangananche akwiga, kehayo akalichoka komaha oyo akubina irina ree. Hano akuhika hangi, umwiseke ora agakira, Wesanganache akamuburia hano arure, umwiseke ora akamotebia, akamanya iga no omona o musubati omobo. Umwiseke ora akamotebia iga nachere iga Wesanganache amogore ichingebo kuejira agoterwa.

Hano bokeye Wesanganache akamotebia iga hano borache bwire, "Uche ogende kurara bori hamwi ni chingombe, ensera oraye, uche omahe eng'ombe eno erache egotache engombe eyo niyo erache ekorwe ichingebo chao". Urusik rokaya igo kuhika bokaira abanto bonswi bakaya korara. Umwiseke ora akaya korara bori, kehara wanyore atebibwi na mamai wabo. Ubatiko gatai, akamaha akangombe kano kaba egetunkwe karacha igo karamotacha.

Inkio hano yahikire akaya gokeria mamai wabo. Hano basokiri gokerania, Wesanganache akamuburia iga, 'mamai engombe nehai Yare egotachere?" Umwiseke ora akagamba iga ni nyamahara erenge hangi ni ndigi. Hano Wesanganche ageruche agaseka akagamba iga mbuya mamai.

Wesanganache agatebia abamura bae igabachinch nyamahara soki baimiki amabiba batore ichinyama choswi ko mabiba baikari riko go kera inyumba. Abamura bara bagakora kehara batebibwi neisowabo.

Hano basokiri, umwiseke ora agatebibwa iga egereri ichinyama chira kuhika chihe chihike atahonyoye. Agasokia kera omonto akagenda mogondo agatama umwiseke ora umwene. Ichinyama chira cikagenderia kohea, chikanyuka buya kemwe kemwe, sibono umwiseke ora taho- nyoye. Hano bugutuna kwiro, abanto bonswi bakaringa gucha ka. Wesanganache agacha akaburia umwiseke ora hanga ahonyoe umwiseke ora akagamba iga tahonyoyehei.

Wesanganache agatebia abamura bae iga bawanse kohonyora amabiba gara. Kera omumura akaya kunymba imwi. Umumura omwi akahonyora akanyora ichingebo cha kera temo oonde akanyora emesanga, oonde akanyora ibirato, oonde akanyora ibitambara. Kera iribiba nderure ibinto. Umwiseke ora agaswara akahuena bokong'u. Hano bokeye agatebia mamai wabo iga atigare buya, akaringa kya wabo ana omiwgwano.

Hano ahikire ka wabo, musubati omobo hano akomomaha kebore asware, akamba iga" uni nendaye omamai gutuna ichingibo. Umwiseke ora anyore ichingebo akamotebia kebore arahike o Wesanganache. Nyakwabo akamosemir ibiakorea bino arare gonchera kuhika ahike omamai wabo, agatanora kuwa o Wesanganache.

Akagenda igo akahika ko gesaka ckenene agasikan cgekondo. Egekondo keno gekamuburia iga "Oromwiseke nowangwi ore?". Umwiseke ora akagetebia. Guiki gekamubu ga nehai ukuya, akamba iga "no Wesanganache nkuya". Egekondo kera gekagamba iga oo maha enchera neyo ikuya ho. Akagenda igo agasikana inyamururai. Inyamururai eno ekamubauria kehara bene egekondo kemubuni, akagetebi Irina lesowabo na hano akuya. Hano agosokia ikamotebia iga maha enchera neyo irakuhire wae.

Akagenderia no rogendo roe. Akagenda igo akahika kunyumba yu umukungu ono akakunguha. Umukungu ora

hano akomomaha akamuburia hano akuya, umwiseke ora akaı tebia iga no Wesanganache akuya. Umukungu ora akamote bia iga hano akuhika o Wesanganache, ahetere gukihita kera kena orotente, atakahetera gonchera inchiya era.

Basi mbe umwiseke ora agatanura, hano akagen hake igo, akagamba ig "niyeke urukungu rono rokangangi ngokanya rore iga nenkagenda korotentente! terohohai rono ngatacha amasai.

Akagenda igo akahika o Wesangana akamaha; enchera inchiya era, akagera ho akahika isiko, akaburi hanga era niyo o Wesanganache, agatebibwa iga niyo. Akorokibwa hara Wesanganache are, akaya komokeria. Akamotebia iga hata we nachere kogorwa ichingebo agote rwa. Wesanganache akagamba iga mbuya mamai.

Hano gukuhika omogoroba, Wesanganche akamote iga hano abande barayi korara, agende kurara bori amah en'ombe eno erache emotache niyo erache ikorwe Ichingi chaee. Umwiseke ora akarogora kebore arayi korara bori aranunkerwa ne ichingombe ne mbeho iramwita. Han abande bagosoha korana akagenda bori, akaya akaimera i hano akoma nya iga abande baraye akaringa gucha nyumba kurara.

Inkio chuni akaya gokeria mamai wabo. Hano bagosokia gokerania, Wesanganache, akamuburia iga, "Engombe nehai yare egotachere?" Umwiseke ora akamoroki

ogotang'ana ogonene gora. Wesanganache akagamba iga mbuya

Agatebia abamura bae iga bagote engombe era bagichinche soki bakore kehara bakore engaki era ya mbere. Hano basokiri gokora kehara sowabo abatebiri, bagtebia umwiseke ora iga, emenemo gee nokuegereria ichinyama chira chike chihike atahonyoye. Hano bagosokia komotebia, kera omonto akaimika irichembe akaya magondo. Umwiseke ora agatama umwene. Ichinyama chira chikawansa kohea, bebore chavekogenderia kohea, nkeho chate kunyunka buya. Hano chigutuna kohea kimwi, chikanyunka buya bokangu, umwiseke ora akanga kugumiria. Akaya gokera inyumba hano ahika ahonyora amiikia inyama akera sokia akundikiria. Agokora kehayo bene kuhika akohonyora amabiba gonswi.

Engaki ekahika, abanto bonswi bakainoka kurwa mogondo bagacha ka. Wesanganache hano achere, akaburia umwiseke ora hanga ahonyoye amabiba gara, umwiseke ora, akagamba iga tahonyoye. Agatebia abamura bae iga kera omumura ahonyore iribia amahe keno kemo. Hano bahonyoye mbarugore. Oonde akanyora amato, oonde akanyora amagena abande tebonyore gento kwibiba. Umwiseke ora akahabwa amato na magena gara akaringa kuya wabo arakura.

Irigano rene hayo rehekeye.

GOKO NA ABANA

Karai hayo nkanyora Umukungu onde aho. Umukungu oyo Kanyora nana Umumura ono arenge na abana abaru. Gukugira Yubukunguhu boe, umukungu oyo we tare kuya mogondo sibono nare gutigwa ka hamwi na bachokoro bae hano abande baya mogondo.

Umukungu oyo kura nkanyora aba irinani. Hanc amaha iga kera omonto ageye mogondo awansa kubimba keng ng'ora igo kuhika aba irinani, irinene bokong'u. Ukubi koyo nkore kobohia bachokoro bae. Gukugira eyo mbare gukura na gokora igituri sibono teonto are kuigwa kugira omogondo hano sowabo na nyakwabo bare kurema na harai gole.

Orusiku ronde abana bayo bakamaha iga goko wabo abahaye inyanyi bokon'gu bkairusia gotebia isowabo kebore goko wabo akuya arabimba kengora igo kuhika aba irinani. Royo nigo isowabo ahikire igo bakamotebia. Isowabo hano aigure amangana gayo, nangere kemwe akagam iga "mbe! bare bana oyo mbaba mogotoka, gukurua rohei Baba abaye irinani? niche mbateme hamwi na nyakowenyu nyora newe abatebia igo".

Nenkanyora isowabo abatebiri iga narabateme, tebobohere kogamba iga goko wabo kubimba are igo aba irinani. Gukugira eyo, isowabo akagamba iga naraimahere umwene.

Inkio hara isowabo na nyakwabo abana bara bagatanora kuya mogondo. Hono bakuhika ahase nyaborebe, Isowabo abana bara akaringa agacha akaigunya nyuma yinyumba

Umukungu ora agakanya Iga bageye mogondo kohayo akamanya iga naragenderi ne meremo gee.

Hano ichinsa chahetere nke igo Umukungu Ora akawansa kubimba kengora. Kebore arenge kubimba nkeho abana bare gukura na gukenya kuya hano na hara. Umukungu ora akagenderia kubimba kuhika akaba irinani irinene bokon'gu hata isowabo abana bara akoboha. Hano Umukungu oyo asokiri kubimba sowabo abana bara akarua hara wanyore aigunyere agacha aharabu. Umukungu ora hano aroche iga amanyerwe akoboha bokong'u orusiko ronde akabimba igo akaba Inchugu enene bokong'u akaya komenya gesaka.

Gukuma hayo mbaka neno abakuria tebakorea inchuquhai. Nkoqamba bane iqa inchugu ngoko wabo.

Irigano rene hayo rehekeye.

TAFSIRI YA NGANO ZA WAKURIA

MAMA NA SUNGURA

Hapo zamani za kale, kulikuwako na mama mmc Siku moja akazaa moto. Kwa sababu hakuwa na mtu wa kumlea moto wake alikuwa akienda kila mahali na mtotc wake. Akienda shambani, mtoto yuko mgongoni, vivyo hivyo mtoni kuteka maji na msituni kukusanya kuni.

Siku moja akaenda shambani na mtoto, pale shambani alimkalisha mtoto wake chini akaanza kulima. Mara tu akatokea sungura akipita karibu na shamba la yule mama. Sungura alipoona mtoto wa yule mama alivy mzuri na mwenye afya akatamani kumfanya kitoweo. Mai moja sungura akasema "ala! huyu ni mama gani asiyekuv na mlezi wa mtoto wake?, kana kwamba hakuna walezi s hizi". Yule mama akasema "tafadhali kaka sungura kuv mlezi wa mtoto wangu.

Sungura aliposikia hivyo alifurahi sana. A aenda karibu na yule mtoto akambeba na kuanza kumwimb nyimbo tamutamu, hata yule mama akafurahi sana. Sasa alijua kuwa ataweza kufanya shughuli zake zote kwa urahisi sana.

Siku zilipita nyingi, sungura bado akiwa ar shi kwa yule mama akifanya kazi yake ya kulea mtoto. Yule mama alikuwa akimwachia sungura mtoto na kuenda kufanya kazi zake. Sungura naye kwa upande wake lich ya kuwa na nia mbaya alijitahidi kuwa mlezi mzuri.

Mama mtoto siku moja aliamka mapema sana kwenda shambani. Akamwita sungura akamwambia kuwa hatawahi kurudi nyumbani mapema, kwa hivyo itambidi sungura kuangalia mtoto vizuri alale asimsumbue sana. Baada ya hayo yule mama akaondoka.

Yule mama alipotoka tu, sungura akamweka mtoto chini akaanza kukusanya kuni na kupuliza moto. Alipomaliza kupuliza moto, akachukua kisu akakinoa vilivyo kikawa na makali kama wembe. Baada ya kufanya hivyo akaenda akamchukua yule mtoto akamchinja, akatoboa tumbo lake, akatoa maini pamoja na matumbo, kisha akapeleka mabaki ya yule mtoto kitandani akafunika vizuri akarudi kuchoma maini pamoja na matumbo. Akayachoma vizuri, yalipokuwa tayari akakaa kula. Aliposhiba, akachukua yaliyobaki akmwekea yule mama.

Ilipofika adhuhuri, mama mtoto akarudi nyumba Sungura alipomwona tu, akatimua mbio kwenda kwake akise "eh! eh! leo mtoto hakunisumbua, amelala kweli kweli. Nilimwosha vizuri kisha nikamlisha ndiyo maana amelala hivyo. Hata wewe hauna haja kumnyonyesha, amelala na nafikiri hataamka haraka". Yule mama akapewa kiti n sungura. Mara moja sungura akamletea maini yaliyochomw Mama mtoto akamuliza sungura "maini haya umetoa wapi?" Sungura akamjibu "nimepewa na wawindaji". Basi yule mama bila kusita akaanza kula.

Lakini sungura akaanza kuimba akisema,

mwenye kula maini ya mtoto wake

mwenye kula maini ya mtoto wake

Yule mama aliposikia maneno hayo akamwuliza Sungura "unaimbaje?" Sungura akanyamaza. Mama mtoto akaanza kula tena, lakini sungura akarudia maneno yale yale akiimba.

Sasa mama yule akaacha kula, akamwita sungura lakini sungura akakataa kwenda karibu naye. Badala ya sungura alianza kupita mbali na yule mama. Mama yule akaingia ndani ya nymba na kuenda hadi kitandani. Aliposhika mtoto, akakuta kwamba mtoto alikufa kitambo na ametolewa matumbo yote. Hapo ndipo alitambua sabab ya sungura kuimba vile. Alikuwa anakula maini ya mtot wake. Akatoka nje kwenda kumfukuza sungura. Akitoke hapa, sungura naye alikimbia kwenda upande mwingine. Akifika karibu sana na sungura, sungura anaimba hivi.

Umeshika kizingiti

Nitaambia wazee

Akamfukuza sungura kwa muda mrefu lakini hakumshika. Sungura alikimbia na kuingia vichakani, akamwacha mama mtoto analia.

Ngano yangu imeishia hapo.

WESANGANACHE

Hapo zamani za kale kulikuwako na mzee mmoja ambaye aliitwa Wesanganache. Mzee huyu alikuwa tajiri kwa kila kitu. Ingawa yeye alikuwa tajiri, dada yake hakuwa na kitu chochote cha maana kwa sababu mumewe alikuwa masikini sana. Huyu dada yake alikuwa na binti wawili ambao walikuwa hawana nguo nzuri za kuvaa. Huyu dada yake Wesanganache akakaa akafikiri sana, hata mwisho akafikia uamzi kuwa mtu wa pekee ambaye angemsaidia ni kaka yake Wesanganache. Baada ya kufikia uamzi huo, alimwambia mumewe, na wote wakakubaliana kuwa binti yao wa kwanza aende kwa mjomba wake kutafuta nguo.

Huyo msichana akatayarishiwa chakula cha kula njiani na mama yake wakati akisafiri kwenda kwa mjomba wake. Siku ilipofika ya kuondoka, alwaaga wazazi na dada yake akaanza safari yake. Akatembea kwa muda mrefu sana, akafika kwenye chaka kubwa sana. Hapo akakutana na kima. Huyu kima akamwuliza, "wewe msichana baba yako anaitwa nani?" Yule msichana akamwambia jina la baba yake. Tena akamwuliza "unaenda wapi?" yule msichana akamjibu kwa wimbo akaimba hivi,

Nauliza kwa Wesanganache
Kama hataniua anifanye mke
Niwe napika chakula na kumpelekea.

Alipomaliza kuimba, yule kima akasema

UNIVERSITY OF ...

"Kumbe unaenda kuwa Wesanganache! angalia njia ya kwenda kwake, ndiyo hiyo. Yule msichana akaifuata njia aliyoonyeshwa na kima. Akaenda hadi akavuka ng'ambo ya pili. Huko akakutana na fisi. Fisi naye akamwuliza, "Wewe msichana baba yako anaitwa nani?" Yule msichana akamwambia, tena akamwuliza "Unaenda wapi?", akamjibu kwa kuimba wimbo wake ule ule ambao aliutumia kumjibu Kima. Fisi naye akamwambia, "kumbe unaenda kwa Wesanganche, angalia njia ndiyo ile itakayo kupeleka hadi kwake". Yule msichana akaendelea na safari yake. Kila alipokutana na mtu au mnyama, aliwajibu na kuwaambia anapoenda kwa kutumia wimbo huo huo.

Alipokuwa karibu kufika kwa Wesanganche alikutana na mama mmoja aliyekuwa amezeeka vilivyo, Alipomwona huyu kibibi aliende akamsalimia. Yule kibibi naye akamwuliza mahali anapoenda, yule msichana akasema kuwa anaenda kwa Wesanganache. Kibibi akamwonyesha njia pamoja na kumwambia vile ataingia kwenye mji huo. Kibibi alimwambia kuwa, akifika karibu na mji wa Wesanganache, afuate njia yenye samadi badala ya njia nzuri. Alipofika kwa mji wenyewe alifuata njia yenye samadi. Mara tu alipofika uani alianza kuimba wimbo wake akisema

Nauliza kwa Wesanganache
Kama hataniua, anifanye mke
Niwe napika chakula na kumpelekea.

Wesanganache aliposikia wimbo huo alitoka nje ili aone huyo anayeimba akitaja jina lake. Alipofika karibu, yule msichana akanyamaza. Wesanganache akamwuliza mahali anapotoka, msichana akamwambia, tena akamwuliza jina la baba na mama yake, akamwambia, na hapo Wesanganache akatambua kuwa yule msichana alikuwa mtoto wa dada yake. Msichana yule akamwambia Wesanganache shida yake. Alimwambia kuwa shida yake ilikuwa nguo, hivyo alitaka Wesanganache amnunulie nguo.

Kesho yake Wesanganache akamwambia kuwa, usiku ukiingia, asiende kulala pamoja na wasichana wengine, bali aende kulala kwenye zizi la ngombe. Atakapokuwa huko huko achunge ngombe atakaye mkanyaga. Huyo ngombe ndiye atakuwa nguo. Usiku ulipofika yule msichana alifanya kama alivyoelezwa na mjomba wake. Usiku wa manane alishitushwa na ngombe aliyemkanyaga. Ng'ombe huyu alikuwa amekonda vilivyo.

Asubuhi yule msichana aliamka kwenda kumsalimia mjomba wake. Baada ya kuamkiana, Wesanganache alimwuliza "ni ngombe gani aliyekukanyaga?" Yule msichana akamwonyesha. Wesanganache alipomwona ng'ombe huyo, alicheka na kusema ni vyema.

Wesanganache akawaambia vijana wake kuwa wamchinje huyo ngombe, kisha wachukue nyama zote na kuzitia kwenye mapipa mengi. Kila pipa liliwekwa nyama na kuwekwa

hapa alikutana na kima. Kima akamwuliza "wewe msichana unaenda wapi?". Akamjibu kwa kusema, ninaenda kwa Wesanganache. Yule kima akasema "Kumbe unaenda kwa Wesanganache, angalia njia ya kwenda huko ndiyo hiyo". Yule msichana akaifuata. Akaenda hadi akakutana na fisi, fisi naye akamwuliza, "wewe msichana, baba yako anaitwa nani?", yule msichana akamwambia, tena fisi akamwuliza, "unaenda wapi?" akamjibu kuwa anaenda kwa Wesanganache. Fisi naye akasema, shika njia hiyo hapo itakufikisha kwake.

Baada ya kuzungumza na fisi, yule msichana aliishika njia aliyoonyeshwa na fisi akaendelea na safari yake. Akaenda kwa muda mrefu, ndipo akakutana na kibibi mzee. Huyu kibibi akamwuliza "mtoto wangu unaenda wapi?". Msichana yule akasema kuwa, "ninaenda kwa Wesanganache. Kibibi kusikia hivyo akasema, "angalia njia inayoenda huko ni hii, lakini ukifika huko usipitie kwa njia nzuri, bali pitia kwa njia ile yenye samadi". Basi msichana akaendelea na safari yake tena. Alipofika mahali fulani akasema, "kweli huyu kibibi ni mjinga sana. Anafikiri mimi naweza kukanyaga samadi!" Akaendelea na safari yake hadi akafika karibu na mji wenyewe. Alipofika, aliishika njia nzuri isiyokuwa na samadi hadi akaingia nyumbani kwa Wesanganache. Akaonyeshwa alipokuwa Wesanganache akaenda kumsalimia. Baada ya salamu, Wesanganache alimwuliza majina ya wazazi

wake. Alipomwambia, alijua kuwa huyu alikuwa mtoto wa dada yake. Yule msichana akamwambia kuwa amekuja kutafuta nguo. Wesanganache akasema ni vyema. Jioni ilipofika Wesanganache akamwambia kuwa usiku ukiingia, asiende kulala na wengine, badala yake aende kulala kwenye zizi la ngombe. Atakapokuwa amelala achunge ngombe atakayemkanyaga. Huyo ngombe ndiye atakuwa nguo zake. Yule msichana alishangaa sana kwa kuwa hakupata kusikia kuwa mtu analala zizini pamoja na ngombe.

Usiku ulipoingina, wengine walienda kulala kama kawaida, na yule msichana akaenda kule zizini. Al fika huko, hakuvumilia baridi na harufu mbaya ya ngombe Alichofanya ni kwamba, alingojea hadi kila mtu akalala kisha akarudi polepole ndani ya nyumba akalala hadi asubuhi. Asubuhi na mapema akaamka kwenda kumwamkia mjomba wake. Baada ya salamu, Wesenganache akamwuliza hivi "ni ngombe gani aliyekukanyaga?". Yule msichana akamwonyesha yule ndume mkubwa kuliko wote. Wesanganac akasema kuwa ni vyema.

Mara moja akawaambia vijana wake wamshike ngombe huyo, wamchinje kisha wamfanye kama walivyo mfan yule wa kwanza. Baada ya kumaliza wakamwambia yule msichana kuwa kazi yake itakuwa ni kuchochea moto peke yake. Pia wakamwonya kuwa asije akafunua mapipa hata kidogo.

Baada ya kumwambia hivyo, kila mtu akaondoka kwenda shambani, akabakia yule msichana peke yake. Zile nyama zikaanza kuchemka na yule msichana akaendelea kuchochea moto. Zilipokuwa karibu kuiva zikanukia vizuri sana. Yule msichana hakuweza kuvumilia, akaamua kufunua kila pipa na kuonja ili kuhakikisha kama zimeiva, kisha akafunika.

Alipomaliza kufanya hivyo, watu waliokuwa wame-enda shambani, wakarejea nyumbani. Wesanganche alipofika alimwuliza yule msichana kama amefunua mapipa. Yule msichana akakataa. Basi Wesanganache akawaambia vijana wake wafunue yale mapipa, kila kijana akienda kwenye nyumba moja. Walipofunua mapipa yale walishangaa. Kijana wa kwanza alipofungua alipata majani na mtawi, wa pili akapata mawe, wa tatu akapata ngozi ngumu kweli kweli na wengine hawakupata kitu chochote.

Yule msichana akavalishwa ile ngozi ngumu, akafungiwa majani, matawi na mawe akarudi kwao akilia na mwenye huzuni.

Ngano yangu imeishia hapo.

NYANYA NA WATOTO

Hapo zamani za kale, paliondokea mama mmoja ambaye alikuwa anaishi na mwanawe. Huyu mwanawe alikuwa na mke pamoja na watoto wengi. Kwa sababu huyu mama alikuwa mkongwe sana, hakuweza kwenda shambani pamoja

UNIVER... ...KOBI

na wengine. Kwa sababu hiyo alibakia nyumbani na watoto, wakati watu wengine walipoenda shambani.

Kila siku walipoondoka, mama mzee huyu alikuwa anaanza kufura pole pole anabadilika na kuwa kiumbe mwingine mwenye kutisha. Kumbe alikuwa amegeuka na kuwa zimwi. Hali hii ya kufura na kugeuka ilikuwa inawatisha na kuwaogofya watoto sana. Kwa sababu hii, watoto walikaa wakilia na kukimbia hapa na pale wakipiga makele. Hata hivyo hakuna aliyeweza kuwasikia kwa sababu shambani kwa wazazi wao kulikuwa mbali sana.

Siku moja, wale watoto wakaamua kumwambia baba yao juu ya kufura na kugeuka kwa nyanya yao. Baba yao alipofika kutoka shambani, wakamwelezea kuwa, nyanya yao kila siku hufura polepole na kugeuka kuwa zimwi. Baba yao hakuamini. Alikataa katakata akasema "ala watoto mbona mnatukana mama yangu, tangu lini mama yangu akawa zimwi, nitakuja niwachape pamoja na mama yenu kama yeye ndiye amewaambia hivyo".

Ingawa Baba yao hakukubali maneno yao, aliamua kuchunguza mambo yalivyo. Asubuhi kama kawaida, watu walijitayarisha kwenda shambani. Walipomaliza matayarisho yao, waliondoka. Walipofika mahali fulani, yule baba watoto akarudi akaja karibu na mji akajificha nyuma ya nyumba.

Yule mama mzee akangojea watu wafike shambani.

Alipohakikisha kuwa kila mtu amefika shambani, alitoka nje akiwa na furaha kwa kuwa ataendesha kazi yake, ya kufura na kuwa zimwi kubwa lenye kuwatisha wale watoto Basi pale nje alianza kujifurisha polepole. Alivyoendelea kunenepa, ndivyo watoto walivyo endelea kuogopa. Alipo-fikia kwango kile cha zimwi hasa, watoto walianza kulia kwa sauti kubwa na kuanza kuanza kukimbia hapa na pale.

Baba yao baada ya kushuhudia jambo hili, hata yeye mwenyewe aliogopa sana. Hata hivyo alijitokeza kutoka pale, alipokuwa amejificha na akaonekana. Mama yake alipomwona alijua kuwa kazi yake mbaya imejulikana. Kwa sababu hii aliogopa sana. Siku moja alifura polepole akawa jitu kubwa sana, kisha akajigeuza kuwa ndovu, mkubwa sana, akakimbia kwenda vichakani. Kuanzia siku hiyo hadi sasa Wakuria hawatumii nyama ya ndovu, kwa sababu wanasema "ndovu ni nyanya yetu".

Ngano yangu imeishia hapo.

MAREJELEO

Akida, H. 1977: "Utamaduni, Matumizi na Misingi ya Lugha ya Kiswahili" Mulika No. 11. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Akivaga na Odaga, 1982: Oral Literature; A School Certificate Course. H.E.B., Nairobi.

Ameir, I.H. 1981: Misingi ya Nadharia ya Fasihi Kimetolewa na Taasisiya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar.

Ameir, I.H. 1983: Fasihi Simulizi Zanzibar. Kimetayarishwa na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Kimetolewa na Tanzania Publishing House. Dar es Salaam.

Bascom, W.R. 1955: "Verbal Art", Makala katika Journal of American Folklore. Toleo la 68.

Chatman, S. 1971: Literary Style. O.U.P. London.

Dorson, R.M. 1973: <u>Folklore and Traditional History.</u> Mounton, Paris.

Finnegan, R. 1970: <u>Oral Literature in Africa</u>. O.U.P. London.

Fischer, E. 1963: <u>The Necessity of Art.</u> Penguin Books, U.K.

Herskovits, M.J. 1958: <u>Dahomean Narratives.</u> New York University Press.

Hymes, D. 1964: <u>Language in Culture and Society.</u> Harper na Row, New York.

Jason, H. na Segal, D. 1977: <u>Patterns in Oral Literature.</u> Mounton, Paris

Khamis, S.A.M. 1983: "Fasihi Simulizi" Makala Katika <u>Mulika No. 15.</u> Jarida la Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

King'ei, G.K. 1982: <u>Uhakiki wa "Nthimo" Methali za Kikamba kwa kufuatia misingi ya methali za Kiswahili.</u> Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Knappert, J. 1975: <u>Myths and Legends of the Swahili.</u> H.E.B. Nairobi.

Kipury, N. (1983): <u>Oral Literature of the Masai</u> H.E.B. Nairobi.

Kirumbi, P.S. 1975: <u>Misingi ya Fasihi Simulizi.</u> Shungwaya Publishers, Nairobi.

Kitingula, B. 1975: Makusanyo ya Fani za Fasihi Simulizi ya Tanzania Bara.

Kitsao, J. 1975: <u>A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts.</u> M.A. Thesis, U.O. N.

Marx na Engels, 1978: <u>On Literature and Art.</u> Progressive Publishers, Moscow.

Matteru, M.L. 1983: "Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili". Makala katika makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Mbele, J. 1980: "Oral Literature and the Writing Tradition". Makala Katika <u>Kiswahil</u> Vol. 50. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Mbiti, J. 1960: Akamba Stories. O.U.P. London.

Mulokozi, M.M. 1983: "Utafiti wa Fasihi Simulizi". Makala katika makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es-Salaam.

Mulokozi, M.M. 1982: "Protest and Resistance in Swahili poetry 1660 - 1885. Makala katika Kiswahili Vol. 49/1 March Jarida la Taasisiya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Nandwa na Bukenya, 1983: Oral Literature for Schools. Longman, Nairobi.

Nandwa, J.A. 1976: Oral Literature Among The Abaluyia M.A. Thesis, U.O.N.

Odaga, A.B. 1984: Yesterday's Today: The Study of Oral Literature. Lake Publishers & Enterprises. Kisumu.

Okpewho, I. 1975: The Aesthetic of Old African Art". Makala katika OKIKE No.8 (Mhariri) Chinua Achebe, Massachusetts.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

P'Bitek, O. 1973: Africans Cultural Revolution
Macmillan, Nairobi.

Robert, S. na Robert, K. 1978: The Nature of Narrative
O.U.P. London.

Vansina, J. 1965: Oral Traditions. Reutled and Kegan
Paul. London.

Vasquez, A.S. 1965: Art and Society. Monthly Review
Press.

Wanjiku Kabira, 1983: The Oral Artist. H.E.B. Nairobi.

Zipes, J. 1979: Breaking the Magic Spell: Radical
Theories of Folk and Fairy Tales.
H.E.B. London.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY